JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2021

## ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE (CSEE) 2021

# 015 ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es salaam, Tanzania

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI .......... iv

1.0 UTANGULIZI .......... 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI .......... 3

2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha .......... 3
2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi .......... 3
2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu .......... 14
2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi .......... 17
2.2.1 Swali la 3: Nguzo za Imani .......... 17
2.2.2 Swali la 4: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu .......... 20
2.2.3 Swali la 5: Familia ya Kiislamu .......... 24
2.2.4 Swali la 6: Haki na Uadilifu katika Uislamu .......... 28
2.2.5 Swali la 7: Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) 32
2.2.6 Swali la 8: Qur'an .......... 36
2.2.7 Swali la 9: Nguzo za Uislamu. .......... 39
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha .......... 44
2.3.1 Swali la 10: Dola ya Kiislamu Madinah .......... 44
2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadithi .......... 52
2.3.3 Swali la 12: Qur'an .......... 56
2.3.4 Swali la 13: Nguzo za Uislamu .......... 62

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA .......... 67

4.0 HITIMISHO .......... 68

5.0 MAPENDEKEZO .......... 68

Kiambatisho .......... 70

## DIBAJI

Taarifa hii ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2021 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika somo hili. Katika taarifa hii uchambuzi umefanyika katika majibu ya watahiniwa kwakuwa mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo watahiniwa hao waliweza kujifunza kwa usahihi na yale ambayo hawakuweza kujifunza katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Sekondari.

Taarifa hii imeweka bayana jinsi ambavyo watahiniwa wameweza kupata alama za juu, wastani na za chini katika kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa waliofanya vizuri na wale waliofanya vibaya zimeoneshwa. Vile vile, sababu mbalimbali zilizochangia baadhi ya watahiniwa kuweza kujibu maswali kwa usahihi zimeelezwa. Miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na; kuelewa vema matakwa ya maswali na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada mbalimbali za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Aidha, uchambuzi umebaini kuwa watahiniwa walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi walikosa maarifa katika baadhi ya mada za somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya maswali. Uchambuzi umebaini pia udhaifu katika kujenga hoja katika kujibu maswali ya kujieleza kwa ufupi na yale yakujieleza kwa insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau wa elimu kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji ili hatimaye kuondoa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii hivyo kuongeza kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika kipindi kijacho.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani na pongezi za dhati kwa wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii ya uchambuzi.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) mwezi Novemba mwaka 2021 katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mtihani huu uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo husika uliotolewa mwaka 2012 kwa kidato cha I hadi IV.

Maswali yaliyotumika katika Mtihani yaliandaliwa kutoka katika mada kumi na nane (18) kati ya ishirini (20) zilizopo katika muhtasari wa somo. Aidha, maswali hayo yaligawanywa katika sehemu tatu; A, B na C zenye jumla ya alama 100. Sehemu A ilikuwa na maswali mawili (1 na 2), sehemu B ilikuwa na maswali saba (3 hadi 9) na sehemu C ilikuwa na maswali manne (10 na 13). Mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu A na B kisha kuchagua maswali matatu kati ya manne ya sehemu C.

Watahiniwa waliosajiliwa kufanya Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2021 walikuwa 78,493. Kati yao watahiniwa 76,137 sawa na asilimia 96.99 walifanya Mtihani. Idadi hii inaonesha ongezeko la wanafunzi 8,261 ikilinganishwa na wanafunzi 67,876 waliofanya Mtihani wa somo hili mwaka 2020. Kati ya watahiniwa 76,137 waliofanya Mtihani mwaka 2021, watahiniwa 35,671 (47.09%) walifaulu katika madaraja mbalimbali. Jedwali lifuatalo linaonesha madaraja ya wanafunzi hao ikilinganishwa na mwaka 2020.

Jedwali Na. 1: Ulinganifu wa Ufaulu kati ya Mwaka 2020 na 2021

| MWAKA | % YA UFAULU | MADARAJA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | A | B | C | D | F |
| 2020 | 24.97 | 0 | 23 | 2,069 | 14,772 | 50,665 |
| 2021 | 47.09 | 3 | 169 | 8,322 | 27,177 | 40,074 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kupanda kwa kiwango cha ufaulu kwa asilimia 22.12 ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 24.97. Kuongezeka kwa ufaulu huo kulichangiwa na kuongezeka kwa uelewa kuhusu dhana ya upimaji wa umahiri kwa wadau na kuakisi kuwepo kwa mabadiliko chanya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Taarifa hii imechambua majibu ya watahiniwa katika kila swali kwa kulinganisha na matakwa ya swali husika na majibu yake na kile ambacho watahiniwa wamejibu. Aidha, sampuli za majibu sahihi na yasiyo sahihi ya watahiniwa zimeambatanishwa kwa lengo la kuonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali. Taarifa hii imebainisha changamoto zilizowakabili wanafunzi katika kujibu maswali hayo ili zifanyiwe kazi. Pamoja na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa, taarifa hii imebainisha ufaulu wa watahiniwa hao katika mada mbalimbali zilizopimwa. Madaraja ya ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu yalikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 2: Madaraja ya Ufaulu: Elimu ya Dini ya Kiislamu

| ALAMA | DARAJA | MAONI |
|---|---|---|
| 75 - 100 | A | Vizuri Zaidi |
| 65 - 74 | B | Vizuri Sana |
| 45 - 64 | C | Vizuri |
| 30 - 44 | D | Inaridhisha |
| 0 - 29 | F | Dhaifu |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa daraja la juu la ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni A na daraja la mwisho ni F. Pamoja na kuwepo kwa madaraja hayo matano ya ufaulu, taarifa hii itatumia madaraja matatu katika kuwasilisha ngazi za ufaulu ambayo ni: vizuri, wastani na dhaifu. Ufaulu utakuwa dhaifu ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali ni 0 hadi 29. Ufaulu utakuwa wa wastani ikiwa watahiniwa waliofaulu katika swali ni kati ya asilimia 30 hadi 64 na ufaulu ni utakuwa mzuri ikiwa asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali hilo ni 65 hadi 100.

Aidha, hitimisho na mapendekezo kutokana na uchambuzi wa majibu ya watahiniwa umetolewa katika sehemu ya mwisho ya taarifa hii. Inatarajiwa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatatumika katika kuimarisha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Elimu ya Dini ya kiislamu kwa watahiniwa na hatimaye kuboresha kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Tathmini ya kila swali imefanyika kwa kubainisha alichotakiwa kufanya mtahiniwa kwa mujibu wa matakwa ya swali, umahiri uliokusudiwa katika swali au kipengele husika, kisha idadi ya watahiniwa waliojibu swali hilo na hali ya ufaulu wa watahiniwa katika kila swali.


## 2.1 SEHEMU A: Majibu ya Kuchagua na Kuoanisha

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (1 na 2). Swali la kwanza lilikuwa la kuchagua jibu sahihi kutoka katika machaguo matano (A, B, C, D na E). Swali hilo lilikuwa na vipengele kumi na tano (15) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1 hivyo swali zima lilikuwa na alama 15. Swali la pili lilikuwa la kuoanisha lenye vipengele vitano (5) ambapo kila kimoja kilikuwa na alama 1 hivyo swali zima lilikuwa na alama 5. Kwa ujumla sehemu hii ilikuwa na alama 20.

### 2.1.1 Swali la 1: Kuchagua Jibu Sahihi

Swali la 1 lilikuwa na vipengele kumi na tano (i) - (xv) vilivyotolewa katika mada za: *Mtazamo wa Uislamu juu ya Elimu, Nguzo za Imani, Njia za Kumjua Mwenyezi Mungu (S.W), Mtazamo wa Uislamu juu ya Dini, Fiqh na Chimbuko la Fiqhi, Mtazamo wa Uislamu juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Qur'an, Sunnah na Hadithi, Nguzo za Uislamu, Historia ya Katika Uislamu* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah*. Mtahiniwa alitakiwa kuchagua jibu sahihi kati ya machaguo matano aliyopewa (A, B, C, D na E) kisha kuandika herufi ya jibu hilo katika kijitabu chake cha kujibia.

Takwimu zinaonesha kuwa swali hili lilijibiwa na watahiniwa 76,169 ambapo kati yao watahiniwa 43,257 (56.8%) walikuwa na ufaulu wa wastani kwakuwa walipata alama 5 hadi 8. Watahiniwa 17,867 (23.5%) walikuwa na ufaulu mzuri kwakuwa walipata alama 9 hadi 15 na watahiniwa 15,045 (19.8%) walikuwa na ufaulu hafifu kwakuwa walipata alama 0 hadi 4. Aidha, watahiniwa 21 kati ya waliofaulu vizuri katika swali hili walipata alama zote 15. Chati Na. 1 imeonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Chati Na. 1 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa ni mzuri kwakuwa asilimia 80.2 walipata alama 5 hadi 15 ikilinganishwa na asilimia 19.8 waliopata alama hafifu.

Watahiniwa hao waliofaulu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada nyingi zilizounda vipengele mbalimbali vya swali na waliweza kubaini matakwa ya vipengele hivyo. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika kila kipengele umefanyika kama ifuatavyo;

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kuonesha tofauti kati ya mtu aliyeelimika na ambaye hajaelimika. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa dhana ya elimu katika mtazamo wa Uislamu na taathira zake. Aidha, watahiniwa walioelewa vema dhana hiyo walichagua jibu sahihi la kipengele hicho ambalo lilikuwa herufi D *Ufanisi katika utendaji wake*. Kwa upande wa watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi, baadhi yao walichagua herufi E *Uwezo wa kujenga hoja na kuchambua*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kipimo au kigezo halisi cha elimu kwa mujibu wa Uislamu ambacho ni "utendaji" na sio "maneno" hivyo chaguo hili halikuwa sahihi.

Wengine walichagua vipotoshi A *Hatua za kielimu alizofikia* B *Wingi wa tafiti alizofanya* na C *Idadi ya miaka aliyotumia vyuoni*. Hoja hizi si sahihi kwakuwa sio vipimo halisi vya kuelimika kwa mtu kwa mujibu

wa Uislamu. Katika Uislamu athari au alama ya kuelimika inazingatiwa katika tabia na mwenendo wa mtu na sio ngazi ya elimu aliyotunukiwa wala idadi ya tafiti au miaka aliyotumia vyuoni. Aidha, mtu anaweza kuwa na Shahada na kuandika tafiti nyingi katika vyuo mbalimbali na bado akawa hajaelimika ikiwa tabia na mwenendo wake wa maisha ni mbaya. Dhana hiyo ndio msingi unaotofautisha elimu katika mtazamo wa Uislamu dhidi ya mitazamo mingine. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya elimu katika mtazamo wa Uislamu hivyo walishindwa kubaini kigezo sahihi kinacho tofautisha baina ya mtu aliyeelimika na ambaye hajaelimika.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha sifa ya mtu aliye na imani kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka dhana ya Imani na sifa za muumini kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi E *Kujua au kuwa na hoja thabiti juu ya anachokiamini*. Watahiniwa waliochagua jibu hilo walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Imani ya Kiislamu hivyo, walitambua sifa muhimu inayomtambulisha muumini wa kweli.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi wengi wao walichagua vipotoshi B *kuwa na uwezo wa kuvumilia maumivu ya maisha* C *Kujizuia na tamaa na mambo ya anasa* na D *Kuwa mpole na mnyenyekevu akitembea ardhini* ambavyo vilitaja sifa zinazonasibishwa na dhana ya imani katika jamii. Hata hivyo sifa hizo hazikuwa mahususi kisheria katika kufafanua dhana ya imani kwa mujibu wa Uislamu bali ni athari za ibada ya subira. Wengine walichagua kipotoshi A *Kukubaliana na mawazo ya jambo linalosadikika* watahiniwa hawa walichanganya dhana ya “imani” na “kusadikika” ambayo inatumiwa na watu wanaopinga kuwepo kwa Mungu na kunasibisha asili ya vitu vyote na maada. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya imani kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

Katika kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kubaini namna ambayo wanadamu wanahisi uwepo wa Mola Muumba katika maisha yao. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutumia maarifa yao kubaini njia ya kwanza ambayo mwanadamu anaitumia kumtambua Mwenyezi Mungu. Watahiniwa walioelewa vema njia za kumjua Mwenyezi Mungu (S.W) walichagua jibu sahihi D *Uwepo wa*

*athari ya fitra katika maumbile yao*. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali na kutambua nafasi ya Fitra katika maumbile ya wanadamu. Aidha,

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki kwa ujumla walishindwa kuzingatia matakwa ya swali na wengine walikosa maarifa kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu. Wengi kati yao walichagua vipotoshi A *Kwa kuwa na akili tofauti na mnyama* na C *Kwa kukosa kupata majibu kuhusu asili yao* ambavyo vilibainisha njia za kiakili katika kumtambua Mwenyezi Mungu na si njia ya hisia kama ilivyoulizwa kwenye swali. Hivyo watahiniwa hawa walishindwa kubaini jibu sahihi kwakuwa walishindwa kuzingatia matakwa ya swali. Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi B *Kwa kukutana na changamoto mbalimbali*. Watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa hiyo ni hoja au njia ya kimazingira. Aidha, waliochagua kipotoshi E *Kwa kuibuka watu waliotoa habari za Mungu* walishindwa kujua kuwa hiyo ni njia ya wahyi kupitia kwa Mitume (A.S). Kwa ujumla watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu njia za kumjua Mwenyezi Mungu na namna zilivyogawanyika.

Kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubainisha hoja inayofafanua sababu ya kutowezekana kwa mtu kuishi bila ya kuwa na Dini kwa mujibu wa Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu walichagua jibu sahihi B *Dini ni utaratibu wa maisha ya mwanadamu*. Watahiniwa hao walielewa vema kuwa Uislamu umetafsiri Dini kuwa ni mfumo wa maisha na kwa sababu hiyo, hakuna mtu anaweza kuishi hapa duniani bila ya kuwa na utaratibu wa maisha.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana ya Dini kwa ujumla. Miongoni mwao walichagua kipotoshi E *Dini ni Imani ya Mungu muumba aliye juu* tafsiri ambayo mtu anaweza kujivua Dini ikiwa atakataa kuamini kuwepo kwa Mungu, hivyo tafsiri hiyo haitoshi kueleza sababu ya uwezekano wa mtu kuishi bila ya Dini. Wengine walichagua vipotoshi A *Sote ni viumbe wa Mwenyezi Mungu* ambayo siyo sababu ya moja kwa moja inayofafanua kutowezekana kuishi bila ya Dini kwa mujibu wa Uislamu bali ni ukweli unaobainisha asili ya viumbe wote na kusisitiza viumbe hao kuchagua Dini ya Uislamu.

Aidha, waliochagua kipotoshi C *Watu wote wanazaliwa na dini za kimila* walishindwa kuelewa kuwa hoja hiyo haikuwa ya kweli kwakuwa iliandikwa katika msingi usiyo sahihi, kwani watu wanazaliwa na Dini ya Kiislamu kwanza. Kadhalika, waliochagua kipotoshi D *Dini ilifundishwa na Malaika wa Mungu* walishindwa kuelewa kuwa hoja hiyo siyo sahihi kwani hakuna Malaika waliolazimisha watu kuwa na Dini, hivyo haibainishi sababu ya kutowezekana kwa watu kuishi bila ya kuwa na Dini. Kwa ujumla, majibu yote ya watahiniwa walioshindwa yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Dini kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu.

Kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubaini maana ya Dini isiyokubalika kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa dhana ya Dini kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu. Jibu sahihi lilikuwa C *Imani ya kuwepo Mola muumba.* Watahiniwa weledi juu ya dhana ya Dini walitambua kuwa maana iliyofafanuliwa katika herufi C ilizingatia mtazamo wa makafiri juu ya dhana ya Dini kwakuwa wao ndio wanaonasibisha dhana hiyo na imani ya kuwepo kwa Mungu.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa juu ya dhana ya Dini kwa ujumla hivyo hawakujua tofauti kati ya maana iliyotolewa na Uislamu dhidi ya iliyotolewa na makafiri. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi A *Uwezo, Mamlaka au Utawala*, B *Itikadi au mfumo wa maisha,* D *Mila inayofuatwa na jamii ya watu* au E *Mfumo wa maisha ya Akhera* ambavyo vyote vilikuwa na maana sahihi za dhana ya Dini kwa mujibu wa Uislamu. Maana hizo zote zimetumika katika Qur’an ambayo ndiyo msingi mkuu wa maarifa katika Dini ya Kiislamu.

Kipengele cha (vi) mtahiniwa alitakiwa kubaini mambo ambayo yanahusu fani ya Fiq’h katika Dini ya Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka maudhui ya fani ya Fiqh kwa ujumla. Watahiniwa walioelewa vema fani ya Fiq’h walijibu kwa usahihi kwa kuchagua herufi A *Maarifa ya hukumu na sheria.* Watahiniwa hao walifahamu kuwa Fiq’h ni fani mahususi inayoshughulika na kutafsiri sheria mbalimbali za Uislamu kutoka kwenye vyanzo vyake ili zitekelezeke katika mazingira mbalimbali.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hicho walionesha kukosa maarifa kuhusu fani ya Fiqh kwa ujumla, hivyo walijibu kipengele hiki kwa kukisia. Miongoni mwao walichagua kipotoshi E *Hadithi na Sunnah za Mtume (S.A.W)* watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa katika fani ya Fiq'h *Hadithi na Sunnah* ni zana zinazotumika kuelekea maudhui makuu ya fani hiyo. Wengine walichagua vipotoshi C *Itikadi ya upweke wa Allah (S.W)* na D *Imani juu ya mambo yasiyoonekana,* ambavyo havikuwa sahihi kwa sababu vilifafanua maudhui ya fani ya Tawhiid. Vile vile, waliochagua kipotoshi B *Historia ya dini ya Uislamu*, walishindwa kuelewa kuwa kipotoshi hiki kilifafanua maudhui ya fani ya Tarekh.

Kipengele cha (vii) mtahiniwa alitakiwa kubaini njia inayokamilisha kupatikana kwa Ijtihaad kama msingi wa sheria za Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua msingi wa Ijtihaad na kubaini asili yake. Jibu sahihi katika kipengele hiki lilikuwa herufi B *Qur'an + Sunnah + Tafsir ya Wanazuoni*. Aidha, watahiniwa waliochagua jibu hilo walielewa vema kuwa Ijtihaad inapatikana baada ya kutafsiriwa Qur'an na Sunnah ili kubainisha mambo ambayo hayajawekwa wazi katika Qur'an na Hadithi.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki baadhi yao walichagua kipotoshi A *Qiyas + Ijmaa + Tafsir ya wanazuoni*, ambacho ndani yake kulikuwa na Qiyas (kupima vitu vinavyowiana) na Ijmaa (makubaliano ya wanazuoni) ambazo ni vipengele katika Ijtihaad hivyo havielezi kupatikana kwa Ijtihaad, kama msingi wa sheria katika Uislamu. Kadhalika, kipotoshi C *Sunnah + Tafsiri ya wanazuoni + Qiyas* hakikuwa sahihi kwa sababu ndani yake kulikuwa na Qiyas badala ya Qur'an. Vile vile, kipotoshi D *Tafsiri ya wanazuoni + Qur'an + Qiyas*, hakikuwa sahihi kwakuwa ndani yake kulikosekana msingi wa Sunnah. Na kipotoshi E *Sunnah + Rai + Tafsir ya wanazuoni* hakikuwa sahihi kwa sababu ndani yake kulikuwa na Ra'i (maoni binafsi ya mwanazuoni) badala ya Qur'an. Kwa ujumla hakuna Ijtihaad bila ya Qur'an na Sunnah kwani hii ndio asili ya sheria zote za Uislamu na Ijtihaad (juhudi ya wanazuoni) inafanyika kwa kuegemea misingi hiyo kwanza.

Kipengele cha (viii) mtahiniwa alitakiwa kubaini lengo kuu la kuamrishwa kusimamisha nguzo tano za Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa dhana ya

nguzo za Uislamu kwa ujumla na nafasi ya nguzo hizo katika maisha ya kila siku. Jibu la swali hili lilikuwa herufi C *Kumuabudu Allah (S.W) katika kila hatua ya maisha*. Watahiniwa waliojibu kwa usahihi walielewa vema dhana ya nguzo za Uislamu na makusudio yake kwa waumini. Watahiniwa hao walielewa kuwa nguzo za Uislamu ni taasisi zinazomwongoza mwanadamu katika nyanja mbalimbali ili kubaki katika lengo la kuumbwa kwake muda wote.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki, walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nguzo za Uislamu kwa ujumla hivyo walishindwa kubaini jibu sahihi. Baadhi yao walichagua kipotoshi A *Kujuana baina ya wakweli na wanafiki*, wathiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa chaguo hili halikuwa sahihi kwakuwa sio lengo mahususi la nguzo za Uislamu kwani hata watu wanafiki huwa wanatekeleza nguzo hizo. Wengine walichagua kipotoshi B *Kuongeza thawabu na kupata pepo ya Allah (s.w)*, ambao ni miongoni mwa mtazamo potofu juu ya nguzo hizo ambao unasababisha kutenganisha miamala mbalimbali ya maisha ya kila siku na dhana ya ibada baada ya watu kuaminishwa kuwa ameshamaliza wajibu wake kwa kufanya nguzo tano za Uislamu ambazo zimefuta madhambi yake yote.

Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi D *Kuwafanya waislamu kuwa imara na wakakamavu*, huu ni katika ufahamu potofu ulioenea katika jamii kuwa Mwenyezi Mungu ametuwekea nguzo tano za Uislamu kuwa sehemu ya mazoezi ili kufanya miili ya watu kuwa imara. Ingawa athari ya ukakamavu inaweza kupatikana katika utekelezaji wa baadhi ya nguzo hizo lakini sio lengo lake kuu. Walikuwepo pia watahiniwa waliochagua kipotoshi E *Kuimarisha uhusiano wetu na malaika wa Allah (s.w).* Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya mafundisho ya msingi ya Uislamu, kwani juhudi za utekelezaji wa maamrisho yote ya Dini ya Kiislamu yanakusudiwa kuimarisha uhusiano baina ya waumini na Mwenyezi Mungu (S.W) na kupata radhi zake.

Kipengele cha (ix) mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo ambalo si faradhi (lazima) kufanyiwa Maiti Muislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka mambo ya msingi anayopaswa kufanyiwa maiti wa Kiislamu kama yalivyobainishwa katika mafundisho sahihi. Jibu sahihi la kipengele hicho lilikuwa herufi D *Kuwekwa kwenye Jeneza*. Watahiniwa walioelewa vizuri mada ya Mambo ya lazima ya kufanyiwa maiti ya Muislamu walichagua jibu hilo

kwa sababu maiti kuwekwa kwenye jeneza ni utamaduni wa watu katika maeneo mbalimbali ingawa inawezekana kuzika bila ya kumuweka kwenye jeneza.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walichagua vipotoshi A *Kuoshwa*, B *Kukafiniwa*, C *Kuswaliwa* na wengine E *Kuzikwa* ambavyo ni katika vitendo vya lazima (faradhi) kwa mujibu wa mafundisho sahihi ya Uislamu. Endapo maiti wa Kiislamu hatofanyiwa kimoja kati ya mambo hayo (yaliyotajwa katika vipotoshi), jamii yote ya Waislamu katika sehemu (eneo) husika itawajibika kwa makosa hayo. Kwa ujumla watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada ya mambo ya lazima kufanyiwa maiti wa Kiislamu.

Katika kipengele cha (x) mtahiniwa alitakiwa kubaini jambo analopaswa kuzingatia muandaaji katika kuandaa sanda ya mtoto. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutumia maarifa ya "kukafini" maiti wa Kiislamu wa jinsia na umri tofauti. Watahiniwa waliokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu namna ya kukafini maiti walichagua jibu B *Kuwa na vipande vitatu kama ya mwanaume,* watahiniwa hao walielewa kuwa sanda ya mtoto huwa haizingatii jinsia yake, hivyo muundo wake unafafana na sanda ya mwanaume na kutofautiana katika vipimo kulingana na mwili wa mtoto aliyefariki.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi waliashiria kukosa maarifa kuhusu namna ya kukafini maiti hivyo, wengi wao walijibu kipengele hiki kwa kukisia. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua herufi A *Jinsi ya mtoto aliyefariki* na C *Uzito na aina ya kitambaa*, ambapo walithibitisha kutokuwa na maarifa kuhusu jinsi ya kumkafini maiti kwani maandalizi ya sanda ya mtoto hayazingatii jinsia yake wala uzito wa kitambaa. Ama, waliochagua herufi D *Kuwa na vipande vitano kama ya mwanamke,* walishindwa kuelewa makusudio ya sanda ya mwanamke kwani sanda ya mwanamke imewekwa vipengele vingi kwa ajili ya kukamilisha stara yake hukumu ambayo hailazimiki kwa mtoto. Wengine walichagua kipotoshi E *Masharti na nguzo za udhu*, hili ni jambo la kuzingatia kwa mtu anayeosha maiti na siyo mtu anayekafini hivyo halikuwa sahihi.

Kipengele cha (xi) mtahiniwa alitakiwa kubaini dondoo moja ambayo haikuwa miongoni mwa adabu za usomaji wa Qur'an. Swali hili lilipima

umahiri wa watahiniwa kuelewa adabu za usomaji wa Qur'an kama zilivyofundishwa katika kitabu chenyewe na Hadithi mbalimbali za Mtume (S.A.W). Aidha, watahiniwa weledi wa Qur'an na mafundisho yake walijibu kipengele hiki kwa kuchagua herufi A *Kuanza upande wa kulia,* kwani msomaji wa Qur'an halazimiki kuanza kulia au kushoto au katikati yake. Msomaji anaweza kuanza kusoma upande wowote na akapata ujumbe (muongozo) uliokusudiwa.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki wengi walichagua kipotoshi E *Kuzingatia makatazo yake.* Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa hiyo ilikuwa miongoni mwa adabu kubwa za usomaji wa Qur'an, ambayo ni jumla ya kuzingatia malengo yake. Msomaji wa Qur'an wakati wote anapaswa kuzingatia maamrisho na makatazo ya kila aya anayoisoma. Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi B *Kuanza na kumlaani sheitwani*, C *Kuanza na Bismillah* na D *Kusoma ukiwa twahara,* ambavyo ni adabu zilizobainishwa moja kwa moja na Qur'an yenyewe. Hivyo watahiniwa waliochagua vipotoshi hivi walionesha kutokuwa na maarifa ya kuhusu Qur'an kwa ujumla.

Kipengele cha (xii) mtahiniwa alitakiwa kubaini kazi kuu ya Sunnah katika Uislamu. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kukumbuka kazi kuu ya Sunna kama ilivyofafanuliwa katika mafundisho ya Uislamu. Watahiniwa waliokuwa na maarifa katika mada ya Maana na umuhimu wa Sunnah na Hadithi walichagua jibu sahihi E *Kuitafsiri Qur'an*. Watahiniwa hao walielewa kuwa Sunnah ni taswira ya Qur'an kivitendo kwakuwa ni tabia na mwenendo wa Mtume (S.A.W) kwa ujumla.

Watahiniwa wengi waliokosa kipengele hiki walichagua kipotoshi D *Kuongeza thawabu* na A *Kuongezea ibada.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kupata thawabu siyo malengo ya ibada yoyote katika Uislamu bali ni malipo ya ziada (bonasi) baada ya mtu kufanya jambo lolote jema na Sunna haiongezei ibada bali inaongoza utekelezaji wa ibada zote katika Uislamu. Ama waliochagua kipotoshi C *Kuhifadhi Hadithi* walishindwa kutofautisha kati ya dhana ya Sunnah na Hadithi kwani kazi ya mahususi ya Hadithi ni kuhifadhi Sunna na si kinyume chake.

Watahiniwa wengine walichagua kipotoshi B *Kufuta dhambi,* watahiniwa hao walishindwa kuelewa vema dhana ya kufutwa kwa

madhambi kuwa ni matokeo ya ziada (bonasi) baada ya mja kuzingatia Sunnah katika kila hatua ya maisha yake na siyo malengo ya Sunnah yenyewe. Zaidi ya hapo, dhana ya kufutwa kwa madhambi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu haina mahusiano ya moja kwa moja na amali za mja isipokuwa ni rehema zake Mwenyezi Mungu pekee. Kwa ujumla watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Sunnah na Hadithi.

Katika kipengele cha (xiii) mtahiniwa alitakiwa kubainisha makusudio ya kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa mafundisho ya msingi ya funga ya Ramadhani ambayo ni nguzo ya nne ya Uislamu inayotekelezwa ndani ya mwezi mmoja katika mwaka. Watahiniwa hodari katika mada ya funga ya Ramadhani walichagua jibu sahihi C *Kujifunza kuchunga mipaka ya Allah (S.W)*. Watahiniwa hawa walielewa vema ufafanuzi huo uliotolewa badala ya maneno "kuwa wacha Mungu" ambayo yametajwa katika Qur'an.

Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ibada ya funga ya Ramadhani hivyo walishindwa kubaini malengo yake. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi E *Kuweza kufutiwa dhambi zetu zote*. Watahiniwa hao walionesha kuathirika na mtazamo potofu unaotokana na kueleweka visivyo dhana ya Funga kwa jamii za Waislamu. Aidha, kufutwa kwa madhambi katika Funga (kama ilivyo katika ibada zingine) ni matokeo ya ziada (bonasi) na inaweza kupatikana ikiwa mtu ameweza kufikia lengo la Funga.

Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi walichagua kipotoshi A *Kuwezesha watu wote kuonja ladha ya njaa*, dhana ambayo si sahihi kwa sababu, pamoja na ulazima wa ibada ya Funga lakini bado inatoa udhuru wa kutekelezwa kwake kwa baadhi ya makundi bila kuzingatia hali zao za maisha hivyo si watu wote wanafunga Ramadhani kama ilivyotajwa kwenye kipotoshi hicho. Zaidi ya hapo, miongoni mwa ambao hawaruhusiwi kufunga wapo pia wenye uwezo mkubwa kiuchumi ambao hawaijui kabisa habari ya njaa.

Waliochagua kipotoshi B *Kuweza kufanana na Ummah uliopita*, walichanganya historia ya Funga na malengo ya ibada hiyo kwani hoja waliyochagua ilifafanua na kuwathibitishia Waislamu kuwa ibada ya

Funga haijaanza kwa umma huu pekee bali ilikuwepo katika jamii zilizopita. Wengine walichagua kipotoshi D *Kuadhimisha kushuka kwa Qur'an*, watahiniwa hao walichanganya hoja inayofafanua utukufu wa mwezi wa Ramadhani na malengo ya Funga, kwani taarifa ya kushuka kwa Qur'an ndani ya mwezi wa Ramadhani inalenga kubainisha utukufu wa mwezi huo na siyo malengo ya ibada ya Funga.

Kipengele cha (xiv) mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu ya ushindi wa Nabii Nuhu (A.S) katika zama zake. Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuelewa dhana ya ushindi kwa mujibu wa Uislamu. Aidha, watahiniwa waliokuwa na uelewa mzuri katika mada ya Historia ya Mitume walioteuliwa waliweza kubaini sababu hiyo na kuchagua jibu sahihi E *Waumini walinusurika na makafiri waliangamia*, kwani miongoni mwa tafsiri za ushindi katika Uislamu ni kupata nusura ya Mwenyezi Mungu (S.W).

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya ushindi kwa mujibu wa Uislamu. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi B *Alifanikiwa kuhamia mji mwingine na watu wake*, jambo ambalo halitafsiri ushindi kwakuwa siyo malengo makuu ya kazi ya aliyoifanya Nabii Nuhu (A.S). Wengine walichagua herufi C *Aliweza kuwaokoa watu wote kwa kutumia Jahazi*, hoja hii inapingana na ukweli wa kihistoria, kwani Nabii Nuhu (A.S) hakuondoka na watu wote kama ilivyotajwa katika kipotoshi hiki bali watu wachache waliomkubali.

Watahiniwa wengine walichagua herufi A *Watu wengi walimkubali na kumuamini*, hoja hii pia inapingana na ukweli wa kihistoria, kwani ujumbe wa Nabii Nuhu (A.S) haukupokelewa na watu wengi wa zama zake pamoja na juhudi kubwa haliyoifanya kwa miaka mingi. Ama, waliochagua kipotoshi D *Aliweza kutumia maji kuwaangamiza wapinzani*, walionesha kukosa maarifa kuhusu mipaka na mamlaka ya Mwenyezi Mungu (S.W) kwani uwezo wa kuadhibu haupo kwa yeyote isipokuwa Mwenyezi Mungu pekee. Hivyo hoja hiyo ilipingana na msingi wa itikadi ya Uislamu.

Kipengele cha (xv) mtahiniwa alitakiwa kubaini sababu ya kuitwa "Jahiliyyah" katika zama kabla ya kuja kwa Mtume (S.A.W). Kipengele hiki kilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua Historia ya Bara Arab kabla ya kuletwa Mtume Muhammad (S.A.W).

Aidha, watahiniwa weledi wa Historia walichagua jibu C *Dunia ilipoteza muongozo sahihi kutoka kwa Muumba*, kwakuwa hoja hiyo ilibainisha kwa muhtasari sifa zote zilizoenea katika wakati huo.

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Historia ya Bara Arab zama za Jahiliyyah hivyo walichagua majibu yao kwa kukisia. Baadhi ya watahiniwa hao walichagua kipotoshi A *Dunia nzima hapakuwa na mafundisho ya dini*, ambalo halikuwa sahihi kwa sababu ilipingana na ukweli wa kihistoria kwani mafundisho ya dini mbalimbali yalikuwepo ingawa mengi yalichanganywa na upotofu. Miongoni mwa mafundisho hayo yalikuwepo mafundisho ya Dini ya Kiyahudi na Ukristo.

Wengine walichagua herufi B *Jamii zilikuwa chini katika Sayansi na Teknolojia*, jambo ambalo ni sahihi kihistoria lakini halikuwa sifa mahususi iliyonasibishwa na ujahiliyah kwani sifa zote zilizotafsiri ujahiliya zilikuwa ni za kijamii (itikadi na utamaduni) na kiuchumi.


Wengine walichagua kipotoshi D *Watu walioshi wakati huo hawakujuana*, hoja hii haikuwa sahihi kwakuwa inapingana na sifa ya mwanadamu kuwa kiumbe wa kijamii ambayo inasababisha kushindwa kujiepusha kujuana na wengine. Ama, waliochagua herufi E *Hapakuwa na mfumo wowote wa kiuchumi na utawala*, walioonesha kukosa maarifa ya msingi ya mahitaji ya mwanadamu kwani haiwezekani kimaumbile kwa wanadamu kuishi bila ya mifumo hiyo.

### 2.1.2 Swali la 2: Nguzo za Uislamu

Swali hili lilitolewa katika mada ndogo ya Zakat, na lilikusudiwa kupima umahiri wa watahiniwa kuelewa viwango mbalimbali vya Nisaab kwa mujibu wa Fiq'hi ya Zakat. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kuoanisha aina za mali zilizokuwa katika orodha A (i) - (v) na viwango vya wajibu vya utoaji wa Zakat (Nisaab) vilivyokuwa orodha B (A) – (G) kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwa kila kipengele katika kijitabu chake cha kujibia.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 76,169 ambapo watahiniwa 14,957 (19.6%) walifaulu vizuri kwa kupata alama 4 na 5. Watahiniwa 45,250 (59.4%) walikuwa na ufaulu wa wastani kwakuwa walipata alama 2 na 3

na watahiniwa 15,962 (21.0%) walikuwa na ufaulu hafifu kwakuwa walipata alama 0 na 1. Aidha, watahiniwa 2,701 walipata alama zote 5. Chati namba 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2

Chati Na. 2 inaonesha kuwa na ufaulu mzuri katika swali kwakuwa asilimia 79.0 ya watahiniwa walifaulu

Watahiniwa hao waliofaulu walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Nguzo za Uislamu hususani Nguzo ya Zakat, hivyo waliweza kuoanisha kwa usahihi vipengele viwili hadi vitano.

Katika kipengele cha (i) mtahiniwa alitakiwa kubaini Nisaab ya mazao ya shambani, ambapo jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa herufi F kilo 666, watahiniwa waliochagua jibu hili walionesha kuelewa vema viwango vya Nisaab kwani mazao hayafanyiwi hesabu ya Zakat mpaka baada ya kuvunwa na kupimwa kama yamefikia uzito uliotajwa au zaidi. Aidha, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua herufi D Tola 7.5. Wathiniwa hao walishindwa kubaini kuwa kipimo cha Tola hakitumiki kwenye kupima viwango vya mazao bali kinatumika kupima uzito wa dhahabu na vito kwa ujumla. Wengine walichagua kipotoshi A *Gram 80* ambacho ni pungufu ya Nisaab ya Dhahabu na vito na haitumiki kama kizio cha vipimo vya mazao ya shambani.

Kipengele cha (ii) mtahiniwa alitakiwa kubaini nisaab ya Dhahabu na Vito, ambapo jibu sahihi la kipengele hiki lilikuwa D *Tola 7.5*. Watahiniwa wengi waliojibu vema kipengele hiki walionesha kuwa na elimu ya viwango halisi vya Nisaab. Watahini walioshindwa kujibu kwa usahihi wengi walichagua herufi A *Gram* 80 ambacho ni kiwango pungufu kwa gram 2.5. Aidha, katika utoaji wa Zakat ya dhahabu na vito kiwango mbadala cha Tola 7.5 ni gram 82.5 na siyo gram 80.

Katika kipengele cha (iii) mtahiniwa alitakiwa kubaini nisaab ya Ng'ombe, ambapo watahiniwa waliokumbuka vema kiwango hicho walichagua herufi C *Thelathini,* tofauti na watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi baadhi yao walichagua herufi B *Ishirini* kwa kukadiriwa wingi wake na wengine walichagua herufi E *Watano* ambacho ni kipimo cha Ngamia. Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walionesha kukosa maarifa kuhusu viwango mahususi vya Nisaab ya wanyama.

Katika kipengele cha (iv) mtahiniwa alitakiwa kubaini Nisaab ya mali ya kuokota ambapo jibu lake lilikuwa herufi G *Thamani yoyote,* kwani mali ya kuokota kwa kiwango chochote ni wajibu kutolewa Zakat. Hivyo watahiniwa mahiri katika mada ya Zakat walielewa vema dhana hii na kuchagua jibu sahihi. Aidha, watahiniwa wengi walioshindwa kujibu kwa usahihi kipengele hiki walichagua herufi D *Tola 7.5* ambacho ni kiwango cha Dhahabu na Vito, hivyo halikuwa jibu sahihi katika kipengele hiki. Wengine walichagua herufi C *Thelathini* ambacho ni kiwango mahususi cha Nisaab ya Ng'ombe, majibu hayo ya watahiniwa yaliashiria kubahatisha majibu kwani hayakuwa na uhusiano kwa wingi wala uchache ikilinganishwa na viwango vingine vilivyotajwa.

Kipengele cha (v) mtahiniwa alitakiwa kubaini Nisaab ya Ngamia, ambapo watahiniwa waliofahamu vema viwango vya Zakat ya wanyama walichagua jibu sahihi E *Watano*, kwakuwa thamani ya Ngamia na ukubwa wake ni tofauti na Ng'ombe. Ama, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hicho walichagua kipotoshi B *Ishirini*. Watahiniwa hao walikadiria ukubwa na upungufu wa Nisaab ya wanyama kwa kumi kumi, kwakuwa kiwango cha Nisaab ya Mbuzi ni 40, Ng'ombe ni 30, hivyo wakakadiria Ngamia kuwa 20.


## 2.2 SEHEMU B: Majibu Mafupi

Sehemu hii ilikuwa na maswali saba ya majibu mafupi, kutoka mada za *Nguzo za Imani, Mfumo wa Jamii ya Kiislamu, Familia ya Kiislamu, Haki na Uadilifu katika Uislamu, Historia ya Uislamu baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) hadi hivi leo, Qur'an* na *Nguzo za Uislamu.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote, ambapo kila swali lilikuwa na alama tano (5) hivyo, jumla ya alama zote zilikuwa 35.

### 2.2.1 Swali la 3: Nguzo za Imani

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutumia hoja mbili na mifano kuelimisha jamii ya watu wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W) kwa madai ya kuwa haonekani. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua udhaifu wa madai ya Makafiri dhidi ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwakuwa haonekani.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 71,568 (94.0%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 3,803 (5.0%) walipata alama za wastani ( 2 hadi 3.5) na watahiniwa 798 (1.0%) walipata alama nzuri (4 hadi 5). Aidha, kati ya watahiniwa waliopata alama hafifu, watahiniwa 69,226 (90%) walipata alama 0. Chati Na. 3 imeonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na. 3:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3

Chati Na. 3 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa hafifu kwakuwa asilimia 94.0 walipata alama za chini na waliofaulu walikuwa asilimia 6.0.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu (0 hadi 1.5) walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu udhaifu wa madai ya Makafiri juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo. Sababu hizo zimejitokeza kulingana na aina ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao katika kujibu swali hili.


Baadhi ya watahiniwa walieleza hoja zinazothibitisha kuwepo wa Mwenyezi Mungu badala ya kubainisha udhaifu wa macho katika kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W). Watahiniwa hao walieleza kuwa; *Nafsi ya mwanadamu (mfano vipawa alivyotunukiwa mwanadamu), Kutofautiana maumbile katika jinsia. Historia ya Mitume pamoja na miujiza yao na Historia ya mwanadamu.* Watahiniwa hawa walionesha kushindwa kubaini matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa wengine walieleza madai mengine ya Makafiri dhidi ya kuwepo kwa Allah (S.W) badala ya kubainisha udhaifu wa macho katika kuthibitisha uwepo wake. Majibu yao yalikuwa: *Mwenyezi Mungu hawezi kudiriki kwa milango ya fahamu na Mwenyezi Mungu hajulikani nasaba yake.* Maelezo hayo pia hayakuwa sahihi kwa sababu hayakujibu swali bali yalitaja hoja zingine miongoni mwa madai ya Makafiri dhidi ya kuwepo kwa Allah (S.W).

Baadhi ya watahiniwa, walitaja ishara mbalimbali za kuwepo kwa Allah (S.W) kama vile: *Umbile la mbingu na ardhi na vyote vilivyomo, kuwepo kwa asubuhi na mchana, kuwepo kwa ushahidi wa jua kuchomoza mashariki na kuzama magharibi, kuwepo na kutokea usiku na mchana* badala ya kueleza udhaifu wa hoja ya kupinga uwepo wa Mwenyezi kwakuwa haonekani.

Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu swali hili, walieleza yafuatayo: *Kutojua umuhimu wa dini, Uwepo wa wahy au ufunuo, Ukiwa na imani kuwa Mwenyezimungu yupo hai, Kuamini vitabu vyake.* Watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa kuhusu nguzo ya kwanza ya Imani kwa ujumla hivyo walieleza mambo mbalimbali waliyodhani kuwa yanahusiana na swali.

Kwa ujumla, watahiniwa wengi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, walishindwa kubaini matakwa ya swali hilo hivyo majibu yao hayakufikia makusudio ya swali. Kundi lingine, walishindwa kujibu kwa usahihi kwakuwa walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya kumuamini Mwenyezi Mungu (S.W). Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.


3 i) Umbile la mbingu na ardhi. mfano Mawingu, Miti, bahari, Majabali. hii ni dalili mojawapo inayo thibitisha kuwepo kwa mwenyezimungu (s.w) kwa madai kuwa haonekani laki watu hawamuoni lakini yeye anawaona na kuna dali ambazo zinathibitisha kuwepo kwake mfano umbile la mbingu na ardhi.

ii) Nafsi ya Mwanadamu. mfano binadamu tumepewa tofauti ya vipaji, rangi, Sura, unene, wembamba, urefu na ufupi. hii ni inajitosheleza kuwa hoja inayothibitisha kuwepo kwa Mwenyezimungu (s.w) kwa madai kuwa haonekani.

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 3

Katika kielelezo Na 3.1 mtahiniwa ametaja kwa ujumla ishara za kuwepo kwa Mwenyezi Mungu (S.W) ambazo zipo katika nafsi ya mwanadamu na maumbile badala ya kuonesha udhaifu wa hoja za wanaopinga kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa madai kuwa haonekani.

Pamoja na watahiniwa wengi kupata ufaulu hafifu katika swali hili, walikuwepo pia watahiniwa wachache waliofaulu. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kumuamini Mwenyezi-Mungu (S.W) na walibaini vema matakwa ya swali. Aidha, majibu sahihi ya swali hilo yalikuwa kama ifuatavyo:


(i) *Siyo kila jambo linaweza kuthibitika kwa macho kwani macho yana udhaifu mfano macho hayawezi kuona kwa usahihi pia hayawezi kuona vema kitu kikiwa katika maji, vilevile macho hayawezi kuona vitu vidogo sana mpaka kwa darubini. Hivyo si*

*sahihi kupinga uwepo wa Mungu kwa kuwa hatujawahi kumuona*

(ii) *Kila jambo lina njia na vipimo vyake, kwa mfano hatuwezi kupima urefu kwa kutumia kipima joto au rula kupima hali joto.Vivyo hivyo hatuwezi kupima au kuthibitisha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kwa kumuona kwa macho*

(iii) *Kuwepo kwa mambo au vitu hakutegemei kuonekana kwake pekee, pia milango ya fahamu siyo njia pekee ya kufahamu mambo wakati mwingine mwanadamu anafahamu mambo kwa kutumia mantiki, uzoefu na majaribio kwa mfano tunakubali kuwa dunia ni duara na kwamba inazunguka japo hatujawahi kuiona wala kuhisi mzunguko wake.*

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


3. → Sio kila kitu ambacho hakionekani hakipaswi kuaminiwa kwani kuna vyingine havionekani lakini vipo mfano akili ya mwanadamu haionekani lakini tunaamini juu ya kuwepo kwa. Vivyo hivyo kwa Allah (s.w) haonekani lakini kuna dalili zinazothibitisha uwepo wake.

→ Macho ikiwa kama moja ya milango ya fahamu inaudhaifu mkubwa na ndio maana hatutumii katika kuthibitisha mambo mbalimbali. Mfano kuwepo kwa upepo hakuwezi kukathibitishwa na macho. Vivyo hivyo Allah (s.w) hawezi kudhibitika kwa kutumia milango ya fahamu


Kielelezo Na. 3.2 Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 3

### 2.2.2 Swali la 4: Mfumo wa Jamii ya Kiislamu

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b), kutoka katika mada ndogo ya Misingi ya Maadili katika Uislamu. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza jambo linalowahamasisha Waislamu kusimamia uadilifu katika jamii, na kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kubainisha vyanzo vitatu anavyovitegemea mwanadamu katika kutambua mema na maovu kwa mtazamo wa Uislamu. Swali hili


lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini athari za nguzo za Imani ya Kiislamu kama zinavyotafsirika kivitendo katika maisha ya kila siku.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 50,398 (66.2%) walipata alama hafifu ( 0 hadi 1.5). Watahiniwa 23,751 (31.2%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 2,020 (2.7%) walipata alama nzuri (4 hadi 5). Chati Na. 4 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 4:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, ufaulu katika swali hili ulikuwa wastani kwani asilimia 33.9 ya watahiniwa walipata kati ya alama 2 hadi 5. Wengi kati ya watahiniwa hao waliofaulu, walipata alama za wastani kwakuwa waliweza kubaini matakwa ya swali husika na kutumia maarifa yao kujibu swali hilo ingawa si kwa ukamilifu. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefaulu.



4.a) Jambo linalowahamasisha waislamu kusimamia uadilifu katika jamii ni Uwepo Mwenyezi Mungu

b) i/ kumwamini Mwenyezi Mungu.
ii/ kuamini Vitabu vya Mwenyezi Mungu Unaweza kutambua mema na maovu kwa mtazamo wa Uislamu.
iii/ kuamini Malaika wa Mwenyezi Mungu Unaweza kutambua mema na Maovu kwa Mtazamo wa Uislamu.

Kielelezo Na. 4.1 Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyefaulu Swali la 4

Katika kielelezo Na. 4.1 kipengele (a), mtahiniwa alitoa sababu ya jumla inayowahamasisha Waislamu kusimamia uadilifu katika jamii, kisha kutaja vyanzo vikuu viwili (i na ii) vya utambuzi wa mema na maovu na kutaja kipengele kidogo kimoja (iii) katika chanzo cha tatu. Hivyo mtahiniwa huyo alipata alama nne (4) kati ya tano (5) za swali hilo.

Aidha, majibu sahihi ya swali hilo yalikuwa; (a) Jambo linalowapa hamasa Waislamu kusimamia Uadilifu katika jamii ni matarajio yao ya kupata radhi za Mwenyezi-Mungu na hofu yao juu ya ghadhabu zake. Katika kipengele (b) Vyanzo anavyotegemea mwanadamu kutambua mambo mema na maovu ni: (i) Mwenyezi-Mungu (S.W) (ii) Mitume wa Mwenyezi-Mungu (S.W) na (iii) Vitabu vya Mwenyezi-Mungu (S.W).

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, baadhi yao walishindwa kubaini matakwa ya swali hasa katika kipengele cha kwanza (4a). Wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Misingi ya Uadilifu katika Uislamu ambayo ni tafsiri ya kivitendo ya Nguzo za Imani.  Kwa sababu hizo watahiniwa hao hawakuweza kujibu swali hili ipasavyo.


Miongoni mwa majibu waliyotoa katika kipengele (a) ni kama vile; *Ili jamii iweze kuishi kwa amani na uadilifu, Uadilifu huleta haki na usawa, Maaswi yaliyofanywa na baadhi ya watu mfano mapenzi ya jinsia moja,*

*Mauaji bila ya hatia na sheria yoyote.* Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya kipengele hiki hivyo walitaja mapungufu na changamoto mbalimbali za kijamii kama chanzo cha hamasa ya kusimamia uadilifu.

Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi waliandika yafuatayo; *Dini ya kiislamu, Kuwa wakweli na kutodhulumu mtu katika jamii, Uadilifu ndio nyenzo pekee ya kumuweka muislamu katika imani ya kweli, Uadilifu huleta haki na usawa, Harakati za kusimamisha uislamu.* Majibu haya yalionesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu misingi ya uadilifu katika Uislamu.

Katika kipengele 4(b) ambacho mtahiniwa alitakiwa kubainisha vyanzo vitatu anavyotegemea mwanadamu kutambua mema na maovu kwa mtazamo wa Uislamu. Baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja vipawa alivyotunukiwa mwanadamu na Mwenyezi Mungu (S.W) kama vyanzo vya kutambua mema na maovu. Watahiniwa hao waliandika: *Akili, Elimu na Utambuzi, Mwanadamu anafahamu mema na maovu kwa vipawa alivyotunukiwa, Mwanadamu anatambua mema na maovu kwa kupitia umri aliokuwa nao, Utambuzi binafsi, Uwezo wa kuelimika na kuelimisha*. Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali husika.

Watahiniwa wengine walioshindwa katika kipengele 4(b) walieleza njia za kuthibitisha Shahada badala ya vyanzo vya kutambua mema na maovu. Watahiniwa hao waliandika; *Moyoni, Matamshi na vitendo*. Wengine walifafanua hatua anazopitia mwanadamu kuelekea maisha ya Akhera kama vile: *Siku ya kufa, Kaburini, na siku ya hesabu (Kiyama) maana wema na waovu hujulikana siku hiyo*. Wengine waliandika nyenzo anazotumia mwanadamu kujielimisha kama vile; *Milango ya fahamu na Elimu.* Watahiniwa hawa wote walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu vyanzo vya utambuzi wa mema na maovu hivyo walijibu kipengele hiki kwa kukisia. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


4) a/ jambo ambalo linawahamasisha Waislamu kusimamia
Uadilifu katika jamii ni haki

b/ i/ Ijtihadi
ii/ Qiyaas
iii/ Ijmaa


Kielelezo Na. 4.2 Sampuli Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 4

Katika kielelezo namba 4.2 kipengele (a) mtahiniwa alishindwa kubaini jambo linalowapa Waislamu hamasa ya kusimamia uadilifu na kutaja dhana ya “haki” ambayo haikuwa na maelezo yoyote kiufafanuzi. Aidha, katika kipengele (b) mtahiniwa alitaja baadhi ya misingi ya Fiqh badala ya vyanzo vya utambuzi wa mema na maovu kwa mtazamo wa Uislamu.

### 2.2.3 Swali la 5: Familia ya Kiislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutofautisha kwa kutumia hoja moja kati ya talaka ya Zihaar na talaka ya Li’aan. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua aina mbalimbali za talaka katika sheria za Uislamu.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 76,169 ambapo kati yao watahiniwa 46,795 (61.4%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 18,325 (24.1%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 11,049 (14.5%) walipata alama nzuri (4 hadi 5). Chati Na. 5 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na. 5:** Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5

Chati Na. 5 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani kwakuwa asilimia 38.6 ya walipata alama 2 hadi 5.

Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu talaka katika Uislamu hivyo waliweza kubaini matakwa ya swali hilo na kulijibu ipasavyo. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hilo.


5 Talaka zihaar: ni talaka ya kurejea ambayo inapatik
ana kwa mume kumfananisha mkewe na mamay
ake mzazi Lakini Talaka Li'aan; ni aina ya tal
aka zisizolejewa ambayo hupatika kwa mke au
mume kumfumania mwezie ugoni

Kielelezo Na. 5.1 Sampuli Majibu Sahihi Katika Swali la 5

Katika kielelezo namba 5.1 mtahiniwa aliweza kutofautisha talaka Zihaar na Li’an kwa kuchanganya hoja mbili zunazojibu swali hilo, hoja ya kimaana na aina (hukumu) ingawa majibu yake yalitosheleza zaidi katika kueleza hoja ya kiaina (hukumu) ya talaka hizo. Aidha, maelezo

ya hoja zinazojibu swali hilo kwa ukamilifu yametolewa kama ifuatavyo;

Hoja ya kwanza; Utofauti katika maana ya talaka hizo, nayo ni kama ifuatavyo;

*Talaka ya Zihaar, ni talaka ambayo mume anamsusa (anajitenga na) mke wake kwa kumwambia "Ninakuona kama mgongo wa mama yangu" au kumfananisha na yeyote katika maharimu wake. Jambo ambalo linamuondolea haki (mwanaume) ya kukutana na mwanamke huyo katika tendo la ndoa. Katika talaka hii mume hatoweza kumrejea mke ila kwa kafara.*

*Talaka ya Li'aan hupatikana kwa viapo viwili cha mume na mke, ikiwa mume au mke amemkamata mwenziwe ugoni na hakuna mashahidi wanne walioshuhudia kitendo hicho ila wao wenyewe (kama ni mume amemkamata mkewe). Mume atalazimika kuapa mara nne kuwa anashuhudia kuwa mkewe ni mzinifu na mara yatano ataapa kwamba laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake ikiwa yeye ni miongoni mwa waongo.*

*Mke naye atajitetea kuwa hakufanya kitendo hicho na mara ya tano ataapa kuwa laana ya Allah (s.w) iwe juu yake (imfikie) ikiwa mumewe amesema kweli. Baada ya viapo hivi ndoa huvunjka hapo hapo na hawawezi kurejeana.*

Hoja ya pili ilikuwa; Utofauti katika Aina (Hukumu) nayo inajitokeza katika maelezo yafuatayo;


*Talaka ya Zihaar ni aina ya talaka inayoweza kuvunjwa (kurejea) kwa masharti ya kutoa kafara aidha ya kumuachia mtumwa kuwa huru au kufunga siku sitini mfululizo au kutoa sadaka kwa masikini sitini ikiwa hawezi kufunga kisheria.*

*Talaka ya Li'aan ni aina ya talaka isiyo rejea (haiwezi kuvunjwa) kwani baada ya kiapo cha laana ndoa huvunjika moja kwa moja na hakuna kafara inayoweza kuvunja kiapo hicho na kuirudisha ndoa.*

Watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki na kupata alama hafifu walionesha kukosa maarifa kuhusu mada ya Talaka na Eda. Jambo hilo limedhihirika kutokana na aina ya majibu yaliyotolewa na watahiniwa hao. Miongoni mwao waliandika yafuatayo:

*Talaka Zihaar ni talaka ambayo hutolewa na mwanaume au hutolewa tatu kwa pamoja na Li'aan hutolewa moja au mbili yaani akimaanisha ukajifunze makosa yako alafu urudi kwa mumeo.* Mwingine alijibu:- *Talaka Zihaar ni talaka unamuacha mwanamke kimya kimya na Talaka Li'aan ni aina ya talaka ambayo unampa mwanamke lakini unakuwa unaishi nae nyumba moja chumba tofauti.* Wengine waliojibu; *Talaka Zihaar ni aina ya talaka ambayo anapatiwa mwanamke na baadae kumrejea ikiwa talaka Li'aan ni talaka anayopatiwa mwanamke baada ya kutenda kosa kinyume na makubaliano na kukaa eda.*

Watahiniwa wengine walichanganya maelezo ya aina za talaka na kuandika yafuatayo: *Talaka Zihaar ni talaka ambayo anapopatiwa mume au mke huweza kurejeana na mumewe au mkewe lakini Li'aan ni talaka ambayo akipewa mke wa kiislamu anapaswa kupewa na mume mwingine kwa muda wa siku tisini ndipo arejee kwa mumewe*. Wengine: *Talaka Zihaar ni talaka ambayo mwanamke anadai talaka kwa mumewe na humrudishia mume wake vitu vyote lakini talaka Li'aan ni talaka ambayo mume mwenyewe humpa mke wake talaka na hamrudishii chochote yaani mwanamke hamrudishii mume chochote*. Kwa ujumla majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa walikosa maarifa kuhusu mada ya Talaka na Eda. Kielelezo namba 5.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi.


5 Talaka ya Zihar ni talaka ambayo mwanamke ameachwa ili akajifunze kwao lakini Talaka Lian ni talaka ambayo mwanamke amekubali kujiacha, bila ya kuachwa na mumewe.


Kielelezo Na. 5. Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5

Katika kielelezo Na 5.2 mtahiniwa ameieleza Talaka ya Zihaar kama talaka ya mafunzo kwa mwanamke na Talaka ya Lia'n kama talaka ambayo mwanamke anajivua kwa hiyari yake mwenyewe. Mtahiniwa alikosa maarifa ya kutosha kujua kuwa maelezo aliyoyataja kwenye Zihaar yanapingana na dhana ya Talaka yenyewe. Kadhalika, maelezo aliyoyatoa kwenye Talaka Lia'n yanamaanisha aina nyingine ya Talaka ambayo ni Khuluu (khul) au talaka ya kujivua katika ndoa.

### 2.2.4 Swali la 6: Haki na Uadilifu katika Uislamu

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b), kutoka katika mada ndogo ya Dhana ya Haki na Uadilifu katika Uislamu. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kubainisha nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili katika jamii, na kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kubainisha misingi mitatu inayoweza kuimarisha maadili katika jamii kwa mujibu wa Uislamu. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili katika jamii.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 65,458 (85.9%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 10,270 (13.5%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 441 (0.6%) walipata alama nzuri (4 hadi 5). Aidha, kati ya watahiniwa waliopata alama hafifu, watahiniwa 48,199 (63.3%) walipata alama 0. Chati Na. 6 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao.




**Chati Na 6:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6.*

Chati Na. 6 imeonesha ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali kwakuwa asilimia 85.9 walipata alama hafifu ikilinganishwa na asilimia 14.1 waliopata ufaulu mzuri.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, asilimia 85.9 ya watahiniwa waliopata alama hafifu walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Dhana ya Haki na Uadilifu katika Uislamu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali husika. Kwa sababu hizo, walishindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote vya swali.

Katika kipengele cha 6(a) baadhi ya watahiniwa walieleza maana ya maadili badala ya kueleza nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili, watahiniwa hao walijibu; *Maadili ni utaratibu au mwenendo wa maisha unaofuatwa na jamii husika*. Mwingine alijibu; *Maadili ni kusimamisha nguzo za Uislamu zote tano, mfano kutoa Shahada mbili, kusimamisha Swala, kutoa Zakat, kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhani na kwenda kuhiji.* Mwingine aliandika; *Maadili ni kitendo cha mzazi kumfundisha mtoto wake maadili yenye jinsi ya kutii na kuheshimu watu walio wazima.* Majibu hayo ya watahiniwa yalionesha kushindwa kubaini matakwa ya swali waliloulizwa.

Wengine katika walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja sifa za waumini kama vile; *Awe mchamungu, mkweli, Awe mvumilivu na kuwa na subra*. *Kuwa wakweli na kutodhulumu mtu katika jamii.*

Kundi lingine la watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walieleza umuhimu wa maadili badala ya kubainisha nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili katika jamii: *Ili jamii iweze kuishi kwa amani na uadilifu.* Mwingine alijibu:- *Uadilifu huleta haki na usawa, Uadilifu huleta haki na usawa. Uadilifu ndio nyenzo pekee ya kumuweka muislamu katika imani ya kweli.* Na wengine waliandika madhara ya kukosekana kwa maadili: *Maaswi yaliyofanywa na baadhi ya watu mfano mapenzi ya jinsia moja, Mauaji bila ya hatia na sheria yoyote.*

Baadhi ya watahiniwa walileta majibu ambayo hayahusiani na swali husika, mfano; *Kuwa na dini ya muongozo.* Mwingine; *kuwa na stara.* Mwingine aliandika lengo la ibada ya Swala: *Kumuepusha mwanadamu na mambo ya zinaa.* Mtahiniwa mwingine aliandika kuwa: *Wana nafasi ya kufundisha Stara.* Kwa ujumla watahiniwa hao walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu Dhana ya Haki na Uadilifu katika Uislamu.


Maelezo hayo hayakujibu kwa sahihi matakwa ya swali hilo ambalo mtahiniwa alitakiwa kueleza nafasi ya waislamu katika kusimamisha maadili katika jamii ambayo ni "*Wajibu kwa waislamu kusimamia*

*maadili na mwenendo mwema katika jamii na kupambana na yeyote yule ambae anaeneza ufisadi (uharibifu) kwa watu*." Qur'an (57:25)

Katika kipengele 6(b) mtahiniwa alitakiwa kubainisha misingi mitatu inayoweza kuimarisha maadili katika jamii kwa mujibu wa Uislamu. Baadhi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walitaja misingi au vyanzo vya sheria katika Uislamu badala ya kubainisha misingi ya maadili (uadilifu). Watahiniwa hao waliandika: - *Ijtihaad, Sunnah na Qur'an*.

Wengine walitaja ishara mbalimbali za maadili mema kama vile: *Nidhamu kwa watu wote, Mkarimu kwa wenzake, Avae mavazi mazuri, Kusimamisha Swala, Kutoa Zakat na Sadaka, kufunga Sunnah,* Wengine walijibu; *kusoma Qur'an, Kumswalia Mtume, Upendo huruma na heshima kwa wakubwa na wadogo,* Wengine: *Ukweli, Uadilifu, Uaminifu na Kusimamia haki, Unyenyekevu na Busara*. Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Kundi lingine la watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali hili, waliandika dondoo mbalimbali za kijamii zenye mahusiano na maadili. Miongoni mwa dondoo hizo zilikuwa; *Ndoa, Sheria za dini na misingi ya dini, Elimu ya dini ya Kiislamu, Elimu ya wazazi wote wawili na Elimu ya shuleni.* Licha ya kuwepo kwa mahusiano baina ya dondoo hizo na dhana ya maadili katika jamii, lakini dondoo hizo hazikuwa misingi mahususi ya Uislamu katika maadili. Dondoo walizotaja watahiniwa hao ni njia (wakala) katika kueneza maadili katika jamii. Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


06. a) kujisitili katika mavazi ambayo yana kusitiri wewe maumbele ya sioneka
b) Bainisha misingi mitatu inayoweza kuimarisha maadili katika jamii kwa mujibu wa Uislamu
i) kuvaa mavazi mazuri ambayo yai hayo
ii) kuto kuvaa mavazi macho fu
iii) kujisitili katika mavazi ya sitala zuri

Kielelezo Na. 6.1 Sampuli Majibu Yasiyo Sahihi Katika Swali la 6


Katika kielelezo Na. 6.1 mtahiniwa amefafanua dhana ya maadili kama stara ya mavazi na kuitafsiri dhana hiyo kuwa nafasi ya Waislamu katika kusimamia maadili. Kadhalika, ametaja sifa za mavazi kama misingi inayoweza kuimarisha maadili. Majibu hayo yanaashiria kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya maadili katika mtazamo mpana wa Uislamu.

Pamoja na watahiniwa wengi kuwa na ufaulu hafifu katika swali hili, walikuwepo wachache ambao walionesha kuwa na maarifa kiasi kuhusu Dhana ya Haki na Uadilifu katika mtazamo wa Uislamu. Watahiniwa hao waliweza kubaini matakwa ya swali hilo na kujaribu kutumia maarifa yao kujibu. Hata hivyo hapakuwa na mtahiniwa aliyejibu swali hilo kwa ukamilifu (kama ilivyopaswa) bali walijitahidi kugusa hoja muhimu za swali kwa ujumla. Aidha, majibu sahihi ya swali hilo yalikuwa;

(a) *Ni* ***wajibu*** *kwa Waislamu kusimamia maadili na mwenendo mwema katika jamii na kupambana na yeyote yule ambae anaeneza ufisadi (uharibifu) kwa watu.*

(b) *Misingi mitatu ya kuimarisha maadili (uadilifu) katika Uislamu ni;*
   (i) *Imani juu ya Allah (s.w) (Tawhiid)*
   (ii) *Kuamini kuwepo kwa siku ya mwisho.*
   (iii) *Kuamini nguzo zingine za Imani.*

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefaulu katika swali hili.


6. Nafasi ya waislam ya kusimamia maadili katika jamii ni kuhakikisha kwamba hamna anaeingia maadili katika jamii pia kuna haki inayotendeka ipasavyo.

b) i) Tawhiid
ii) Utume
iii) Imani juu ya siku ya mwisho.


Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya Majibu Sahihi Katika Swali la 6

Katika kielelezo Na. 6.2 mtahiniwa ameeleza kwa ujumla wajibu wa Waislamu katika kusimamia maadili katika jamii na kutaja misingi miwili mikuu (i na iii) na nukta moja kati ya nne zinaunda msingi mkuu wa tatu.

### 2.2.5 Swali la 7: Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W)

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b), kutoka katika mada ndogo ya Ukuaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu wakati wa Makhalifa Wanne Waongofu. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kuthibitisha usahihi wa Khalifa Othmani (R.A) kutumia Zakat na Sadaka ili kuimarisha jeshi la maji. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kubainisha fundisho moja kwa Waislamu kutokana na kadhia iliyotajwa katika kipengele (a). Swali hili lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua mafunzo mbalimbali yatokanayo na historia ya Uislamu baada ya kutawafu Mtume (S.A.W) katika maisha ya kila siku.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 70,883 (93.1%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 4,732 (6.2%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 554 (0.7%) walifaulu vizuri kwa kupata alama (4 hadi 5). Aidha, kati ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu, watahiniwa 63,850 (83.8%) walipata alama 0. Chati Na. 7 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Alama za Watahiniwa katika Swali la 7*

Chati Na. 7 imeonesha ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali kwakuwa asilimia 93.1 walipata alama hafifu ikilinganishwa na asilimia 6.9 waliopata ufaulu mzuri.


Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Historia ya Uislamu baada kutawafu Mtume (S.A.W) na wengine kushindwa kubaini matakwa ya swali. Kwa mfano katika kipengele cha 7(a) watahiniwa hao waliandika;

*Khalifa Othman (R.A) Alitoa Zakat kwa kutakasa nafsi ya mtoaji na nafsi ya mali ya mtoaji* Mwingine alijibu kuwa; *Hawakumuamini Othmani (R.A)* na wengine walijibu *Hawakumpenda katika uongozi wake* na wengine walijibu kuwa; *Khalifa Othmani (R.A) aliwaamrisha waumini wake jambo la Zakat pamoja na sadaka kwa sababu ya kuweza kuwasaidia wasiojiweza*. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini matakwa ya swali kwani badala ya kuthibitisha usahihi wa maamuzi ya Khalifa Othman (R.A) kutumia Zakat na Sadaka katika jeshi wakaeleza malengo ya Zakat na wengine kueleza umuhimu wa kutoa kwa ujumla.

Watahiniwa wengine walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele 7(a) walieleza wasifu wa Othman (R.A) kuwa; *Kiuhalisia kama unaamini uwepo wa Allah na Allah anavyoamrisha na wewe unafuatilia basi na wewe Mwenyezimungu atakusimamia*, wengine walieleza; *Khalifa Othmani (R.A) alikuwa ni mtu ambaye anamtambua sana Mwenyezimungu pia alikuwa anapenda sana kutoa Zakat na Sadaka na kuwahimiza waumini ili waweze kutoa zakat na sadaka kwa ajili ya kuimarisha uislamu kwa ujumla.*

Baadhi ya watahiniwa walieleza Umuhimu na malengo ya Zakat na Sadaka badala ya kuthibitisha usahihi wa alichokifanya Khalifa Othman (R.A), nao walijibu kuwa:- *Zakat na sadaka husafisha nafsi ya mtoaji pamoja na mali yake, Zakat na sadaka hukuza umoja na udugu katika jamii ya waislamu na wengineo, Zakat na sadaka humrudisha mja utu kwa Allah pamoja na mtume wake, Zakat na sadaka humfanya mja kuwa muadilifu, mtenda haki na mwenye huruma kwa wengine na Zakat na sadaka humfanya mja kuacha maovu na kufanya mema pamoja na kuelimisha watu juu ya kufanya mema.* Majibu hayo yaliashiria kuwa watahiniwa walishindwa kubaini matakwa ya swali na hawakuwa na

maarifa ya kutosha katika mada hii. Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kipengele hiki kwa usahihi.


7.(a) Kutumia zakat na sadaqat katika jamii ni
bora kwani watu hunufaika na wengine
hubadilisha mfumo wao wa maisha kuto
ka hali ngumu kabisa na kusogea katika
hali ya afadhali. Khalifa Othman pia alisi
ngumzia kwamba kutumia zago zakat
ni muhimu ili kuimarisha jeshi.


Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7(a)

Katika kielelezo Na. 1 mtahiniwa ameeleza manufaa ya kutoa badala ya kuthibitisha uhalali ama usahihi wa alichokifanya Khalifa Othman katika maamuzi ya matumizi ya Zakat.

Katika kipengele 7(b) ambacho mtahiniwa alitakiwa kutoa mafunzo au mazingatio kutokana na kadhia iliyoelezwa katika kipengele (a), Watahiniwa wengi walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki hawakuwa na maarifa kuhusu mada hii. Sababu hiyo ilidhihirika kutokana na kupishana kwa majibu waliyoyatoa na muktadha wa swali katika kipengele (a). Miongoni mwa majibu hayo ni kama yafuatayo; *Waislamu walipata fundisho kuwa kutoa ni moyo na wala si utajiri, hivyo watu wakawa wanatoa zakat pamoja na sadaka*. Mwingine alijibu kuwa; *Khalifa Othmani (R.A) alifundisha tuwe wachamungu*. Majibu haya yalidhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sehemu ya Historia iliyoulizwa.

Watahiniwa wengine walijibu kuwa: *Ukiwa mtoaji lazima na wewe utapata, kwa hiyo fundisho tunalopata tuwe tunatoa zakat na sadaka.* Na wengine walijibu: *Tuwe wachamungu*. Majibu hayo hayakuwa sahihi kwasababu hayakuakisi muktadha wa swali kwani swali katika kipengele (a) lilikuwa ni tukio la kihistoria lililoibua taharuki katika jamii lakini pamoja na taharuki hiyo Khalifa hakusita kufanya maamuzi yake. Kinyume na majibu yaliyotolewa na watahiniwa walioshindwa ambapo maelezo mengi yalitoa mafunzo kutokana na faida za kutoa kwa

ujumla. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele 7(b).


(b)-kutoa ni katika kipengele cha waislamu.
- Tujifunze kuwa na ~~umani~~ imani na Haki katika uislamu.

Kielezo Na. 2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7(b)

Katika kielelezo Na. 7.2 mtahiniwa ametaja dhana tatu ambazo ameshindwa kuzihusisha na tukio la kihistoria la uamuzi wa kutumia Zakat katika jeshi hivyo majibu yake hayakuakisi tukio hilo la kihistoria.

Hata hivyo, pamoja na watahiniwa wengi kushindwa kujibu kwa usahihi katika swali hilo, walikuwepo watahiniwa wachache waliokaribia majibu sahihi. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kiasi kuhusu Historia katika kipindi cha Makhalifa waongofu ingawa walishindwa kupata alama kamili za swali hilo. Majibu sahihi katika kipengele (a) yalikuwa;


*Khalifah alikuwa sahihi kutumia Zakat na Sadaka katika kuimarisha jeshi kwani jambo hilo linawiana na malengo ya matumizi ya Zakat kulingana na makundi ya mgawanyo wake kwa mujibu wa Qur'an katika kipengele cha kuimarisha (kuilinda) Dini ya Allah (S.W). Hivyo Khalifa Othman (R.A) hakukosea kutumia Zakat na Sadaqa katika kuimarisha jeshi la maji kwani jeshi hilo lilisimama kupigania maslahi ya Dini.*

Katika kipengele (b) ambacho mtahiniwa alitakiwa kutoa fundisho moja kutokana na kadhia iliyotajwa katika kipengele (a). Majibu sahihi yalikuwa; *Mbinu za wanafiki katika kuupiga vita Uislamu kwakuwa hoja hiyo iliibuliwa na wanafiki kwa malengo maovu ya kumchafua Khalifah japokuwa alifanya jambo sahihi kisheria*. *Kuwa na msimamo, Othman (R.A) pamoja na kukosolewa vikali na wanafiki na kufanyiwa propaganda za kumchafua lakini bado hakusita kutekeleza jambo hilo lililokuwa na maslahi makubwa katika Dini.* Majibu hayo yalikuwa sahihi kwasababu kadhia iliyotajwa katika kipengele (a) ni tukio la kihistoria ambalo limetafsiriwa katika namna mbalimbali na wanazuoni.

### 2.2.6 Swali la 8: Qur'an

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kutaja hoja tano zinazothibitisha kuwa Qur'an ilikusanywa na kuandikwa wakati wa Mtume (S.A.W). Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini hatua muhimu katika kukusanywa Qur'an katika msahafu kama ulivyo katika zama hizi.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walijibu swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 69,878 (91.7%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 5,809 (7.6%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 482 walipata alama nzuri (4 hadi 5). Aidha, kati ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu, watahiniwa 58,059 (76.2%) walipata sifuri (0). Chati Na. 8 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Chati Na. 8 imeonesha ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali kwakuwa asilimia 91.7 walipata alama hafifu ikilinganishwa na asilimia 8.3 waliopata ufaulu mzuri.


Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umebaini kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu swali kwa usahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu historia ya Qur'an, hususani Kukusanywa Qur'an katika Msahafu na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Baadhi ya watahiniwa hao walitaja hoja zinazo thibitisha usahihi wa Qur'an kuwa imetoka kwa Allah (S.W), nao waliandika; *Qur'an kushuka kidogo kidogo kwa muda wa miaka 23, Hali aliyokuwa nayo Mtume (s.a.w) wakati wa kupokea wahyi, Kutojua kusoma na kuandika kwa mtume (s.a.w) ,Qur'an yenyewe inathibitisha inatoka kwa Allah (s.w) na kufikishiwa Malaika Jibril (a.s) na kupewa utume Muhammad (s.a.w) na kukosolewa Mtume ndani yake*. Wengine walijibu: *Qur'an ni maneno ya Allah (s.w) yaliyoshushwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w), Ilishushwa kidogo kidogo kwa sababu Mtume (s.a.w) alikuwa hajajua kusoma vizuri, Qur'an ilikusanywa na kuandikwa ili kufikisha ujumbe kwa wanadamu na Qur'an ilishushwa wakati wa Mtume (s.a.w) ili waislamu wapate kujua uwepo wa Allah (s.w).*

Wengine walitaja madai ya makafiri dhidi ya Qur'an, kama vile; *Qur'an ni zao la njozi za Mtume (s.a.w), Qur'an ni zao la anayetaka ufunuo na Qur'an ni mashairi*. Watahiniwa hao walionesha kushindwa kubaini matakwa ya swali ambapo walitakiwa kutaja hoja zinazothibitisha kukusanywa na kuandikwa kwa Qur'an wakati wa Mtume (S.A.W)

Kundi lingine katika walioshindwa kujibu kwa usahihi, walitaja nyenzo za kusadikika na kueleza kuwa zilitumika kuhifadhia Qur'an, nyenzo hizo ni kama vile; *Mifupa, Magome ya miti, Mawe na Ngozi za wanyama.* Majibu hayo hayakuwa sahihi kwa sababu wakati Qur'an inashuka teknolojia ya karatasi ilishakuwepo miaka mingi nyuma yake hivyo hoja hizo zilipingana na ukweli wa kihistoria juu ya kuandikwa na kuhifadhia kwa Qur'an.

Wengine walijibu; *Kupitia hadithi, Kupitia Sunnah, Matini, Isnad na Jahililiyyah*. Wengine walieleza sababu za kuhifadhiwa Qur'an kwa maandishi, kama vile; *kuhofia kufariki kwa mahafidhi, kuhofia kusahau, kuwafundisha wasiojua kukariri, kuwa na waandishi wengi na kuhofia kufariki kwa Mtume (S.A.W).* Majibu hayo ya watahiniwa yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha kuhusu historia ya kukusanywa na kuandikwa Qur'an katika zama za Mtume (S.A.W). Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



i. Kutokujua kusoma kwa mtume (S.a.w)
ii. Mtume alitaka kuwasomea na kuhifadhi maswahaba wake.
iii. Mtume mwenyewe alikuwepo
iv. Kufaadui wa waislamu (makafiri) walitaka kuichafua Qur'an.
v. Hali aliyokuwanao mtume baada ya kupokea wahyi.

Kielelezo 8.1 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 8


Katika kielelezo Na. 8.1 mtahiniwa ametaja hoja zinazothibitisha usahihi wa Qur'an kuwa imetoka kwa Mwenyezi Mungu (S.W) badala ya kuthibitisha kuwa Qur'an ilikusanywa na kuandikwa wakati wa Mtume (S.A.W).

Licha ya watahiniwa wengi kuwa na ufaulu hafifu, walikuwepo wathiniwa wachache waliofaulu vizuri. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa kuhusu mada ya kukusanywa na kuandikwa kwa Qur'an katika msahafu. Hivyo waliweza kutaja hoja zinazothibitisha kuwa Qur'an ilikusanywa na kuandikwa wakati wa Mtume (S.A.W).

Miongoni mwa hoja walizotaja ni pamoja na; *(i) Kwanza kutokuwepo kwa uandishi mkubwa wa hadithi jambo ambalo mtume (S.A.W) alichelea kuwa maswahaba watachanganya Qur'an na hadithi. Hivyo walikusanya Qur'an tu (ii) Mtume (S.A.W) kuwasomea maswahaba Qur'an na kuhifadhi ndani ya vifua vyao (iii) Mtume (S.A.W) kuwataka maswahaba waandike Qur'an kama alivyowasomea (iv) Mtume (s.a.w) aliwataka maswahaba wasome walichoandika ili kutoa hiki kilichoandikwa kama sahihi na (v) Mtume (s.a.w) na maswahaba zake walikusanya na kupanga kwa aya, sura mpaka kukamilika kwake na kuwa kama mashafu ya hivi leo.*

Hoja zingine zinazothibitisha kukusanywa na kuandikwa Qur'an wakati wa Mtume (S.A.W) ni; *(i) Mtume (s.a.w ) alichagua waandishi na kuwaagiza kuandika Qur'an chini ya uangalizi wake kisha akaihakiki,(ii) kuwepo kwa mpangilio mmoja wa sura na aya katika Qur'an tokea uhai wa Mtume (s.a.w) hadi hivi leo, (iii) Kutotofautiana kwa majina ya sura katika Qur'an tokea zama za Maswahaba hadi hivi leo kunabainisha wazi kuwa maswahaba walipokea majina ya sura hizo kutoka kwa Mtume (s.a.w) mwenyewe,(iv) kunakiliwa kwa Qur'an*

*wakati wa khalifa Abubakar (r.a),ambapo Abubakar aliwaagiza baadi ya maswahaba waliokuwa waandishi kufanya kazi ya kunukuu kutoka katika maandishi ambayo tayari yalikwishaandikwa, (v) Hakuna historia ya maswahaba waliohifadhi Qur'an vifuani kutofautiana visomo vyao jambo ambalo linadhihirisha kuwa walikuwa na chanzo kimoja chenye mtiririko unaofanana na (vi) Mtume (s.a.w) kuwakataza Maswahaba wake kuandika hadithi wakati wa mwanzo wa utume.Jambo hili linaonesha namna ambavyo Mtume (s.a.w) alikuwa makini katika uandishi wa Qur'an.* Kielelezo Na 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.



8. (i) Kuanza kutokuwepo kwa uandishi mkubwa wa hadithi jambo ambalo mtume (s.a.w) alichelea kuwa maswahaba watachanganya qur'an na hadithi. Hivyo walikusanya qur'an hii.
(ii). Mtume (s.a.w) kuwa somea Maswahaba qur'an na kuhifadhi ndani ya vifua vyao.
(iii). Mtume (s.a.w) kuwataka Maswahaba waandike qur'an kama alivyowasomea.
(iv). Mtume (s.a.w) aliwataka Maswahaba wasome walichoandika ili kuhakiki kilichoandikwa kama sahihi.
(v) Mtume (s.a.w) na Maswahaba zake kusanyana kupanga, kwa aya, sura mpaka kukamilika kwake na kuwa kama mashafu ya hivi leo.

Kielelezo Na. 8.2 Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 8

### 2.2.7 Swali la 9: Nguzo za Uislamu.

Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b) kutoka katika mada ndogo ya Hijja. Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kubainisha lengo la Hijja na katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi namna ambavyo chumo la haramu linasababisha kutofikiwa lengo la Hijja. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini falsafa ya nguzo ya Hijja katika Uislamu.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 76,169 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 58,033 (76.2%) walipata alama hafifu (0 hadi 1.5). Watahiniwa 16,907 (22.2%) walipata alama za wastani (2 hadi 3.5) na watahiniwa 1,229 (1.9%) walipata alama nzuri (4 hadi 5). Aidha, watahiniwa 44,632 (58.6%) kati ya waliokuwa na ufaulu hafifu walipata sifuri (0). Chati Na. 9 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 9:** *Asilimia ya Alama za Watahiniwa katika Swali la 9*

Chati Na. 9 imeonesha ufaulu hafifu wa watahiniwa katika swali kwakuwa asilimia 76.2 walipata alama hafifu ikilinganishwa na asilimia 23.8 waliopata ufaulu mzuri.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa kwa ujumla umeonesha kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili walikosa maarifa kuhusu Nguzo ya Tano ya Uislamu (Hijja) na wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Katika kipengele (a) watahiniwa hao walichanganya mafunzo ya vitendo vya Hijja na lengo la ibada hiyo, watahiniwa hao waliandika; *Lengo la Hijja ni kuwakumbusha Waislamu kuwa wote ni Ummah mmoja.* Majibu haya ya watahiniwa yaliashiria kueleza athari za vazi la Ihram na kisimamo cha Arafa badala ya kubainisha lengo la Hijja.

Wengine walieleza maana ya Hijja kilugha badala ya kubainisha lengo lake, nao walieleza; *Lengo la Hijja ni kwenda kuzuru nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu (S.W),* na wengine; *Lengo la Hijja ni kwenda kuabudu katika nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu (S.W) kwa wenye uwezo. Kuweza kutufu huko Makka na kuzunguka Al kaaba. Ni kutembelea nyumba takatifu ya Allah (s.w) katika siku na mwezi maalumu iwapo kuna masharti ya Hijjah hiyo.*

Watahiniwa wengine walieleza faida za ibada ya Hijja badala ya lengo la ibada hiyo. Kwa mfano; *Lengo la Hijja ni kwenda kuhiji ili kuondoa madhambi na kuanza kumrudia Mwenyezi Mungu (s.w).* Majibu hayo ya watahiniwa hayakuwa sahihi kwakuwa yalijibiwa kinyume na matakwa ya swali katika kipengele husika. Kwa ujumla watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hicho.

Kundi lingine la wataniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika kipengele hiki walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu ibada ya Hijjah. Watahiniwa hao waliandika maoni mbalimbali kuhusu lengo la Hijja kama vile; *Lengo la Hijja ni kuzunguka katika nyumba ya Al Kaaba ambapo waislamu watazunguka vilima vya Safa na Marwa na kumuomba Allah (S.W) radhi zake (Toba) katika maovu tuliyoyatenda.* Mtahiniwa mwingine alijibu:- *Kufanya umra, kutubu dhambi, kukamilisha nguzo za Uislamu na kupata thawabu.*

Wengine walichanganya lengo la ibada ya Hijja na malengo ya ibada zingine kama vile Swala, Siyam na Zakat. Kwa mfano; *Lengo la ibada ya Hijja ni kumuepusha mja na mambo maovu na machafu* hili ni lengo mahususi la ibada ya Swala sio Hijja. Mwingine alijibu:- *Kumzidishia mtu ucha Mungu* ambalo ni lengo mahususi la ibada ya Funga (Siyam). Wengine walieleza; *Hutakasa mali na nafsi ya muislamu* ambalo ni lengo mahususi la nguzo ya Zakat.

Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi namna ambavyo chumo la haramu linasababisha kutofikiwa lengo la Hijja. Watahiniwa wengi walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hiki. Wengine walishindwa kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha kuhusu nguzo ya Hijja.


Baadhi ya watahiniwa hao walijibu kuwa; *Kutotimiza matakwa ya Hijja kwa misingi ya kiislamu, kutokuwa na lengo la kufanya Hijja, Kutotimiza vipengele vya Hijja*. Majibu haya yalieleza sababu zingine

tofauti na chumo la haramu, hivyo watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali katika kipengele hiki.

Wengine walitoa maana ya chumo la haramu, kama vile; *Chumo la Haramu ni mali ambayo umepata kupitia biashara haramu mfano unauza madawa ya kulevya na ukapata pesa hiyo ni haramu haifai kwenda kuhiji nayo, pia kama mtu ni jambazi amevamia sehemu fulani na kufanikiwa kupata pesa za watu. Hiyo ndiyo maana ya chumo la Haramu.*

Miongoni mwa walioshindwa kujibu kwa sababu ya kukosa maarifa waliandika hoja mbalimbali ambazo hazikuwa na uhusiano na swali kwa ujumla, kama vile; *Kwa sababu waliweza kumkataa Mtume Muhammad (S.A.W) walikuwa wakimtukana na kumpiga na kusanifu mambo anayoyatenda Mtume Muhammad (S.A.W).* Mwingine alitaja makundi ya watu wasiowajibika kuhiji kama vile; *Chumo la haramu linasababisha kutofikiwa lengo la Hijja kama vile mtu hajabaleghe, mtu bado ni mtumwa ambae siyo mtu huru, ambae hana utimamu. Vyote hivi ni vitu ambavyo chumo la haramu linasababisha kutofikiwa lengo la Hijja kwa ujumla pia mtu anatamani kwenda kuhiji lakini hana uwezo.* Majibu hayo ya wathiniwa yaliashiria kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada husika.

Wengine waliandika; *Chumo la haramu halifikishi lengo la Hijja kwani umetumia mali ya haramu kutoka katika nyumba ya Alkaaba na kumuomba Allah radhi zake hali ya kuwa chumo ni haramu lengo la Hijja halitofikiwa. Chumo la Haramu ni mali ya dhuluma, inamkandamiza nafsi ya mtoaji.* Majibu ya watahiniwa hawa yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Hijja. Kielelezo Na. 9.1 kimeonesha mfano wa majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


9 a/ lengo la hijah ni Kumsaidia muhumini au muja kuweza kufutiwa madhambi yake au kutubu kwa Allah (s.w) kama atafuata sheria zote za hijah

9 b/. Chumo la haramu limeweza kutofikia lengo la hijah kwani wato wengi awana uwezo wa kwenda hijah.

Kielelezo 9.1 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 9


Pamoja na watahiniwa wengi kuwa na ufaulu hafifu katika swali hili, walikuwepo watahiniwa wachache waliokuwa na ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Hijja na waliweza kubaini matakwa ya swali katika vipengele vyote viwili.

Majibu sahihi ya swali hili katika kipengele 9(a) yalikuwa; Lengo la Hijja ni *Kumuandaa mja kuwa khalifa wa Allah (S.W) hapa ulimwenguni* **Au** *Kumuandaa mja kumpenda Mola wake kuliko kitu chochote* **Au** *Kumuandaa Muumini kusimamisha Uislamu katika jamii ili kuweka mazingira yatakayomuwezesha kumuabudu Mola wake katika kila kipengele cha maisha ya kibinafsi na kijamii.*

Katika kipengele 9(b) majibu sahihi yalikuwa; *Chumo la haramu linasababisha kutofikiwa kwa lengo la Hijja kwa kuwa asili ya chumo la haramu inatokana na mambo makubwa mawili ambayo ni dhulma na ufisadi (uharibifu). Mambo ambayo mtu aliyehiji anatarajia aje kupambana nayo kuyaondoa katika jamii. Hivyo akiwa mtu ametumia chumo la haramu kwenda kuhiji anakosa mamlaka ya kimaadili katika kupambana na dhulma na ufisadi kwa ujumla kwa kuwa naye anakuwa ni mshiriki wa amali hizo.*

Miongoni mwa watahiniwa waliojibu vizuri kiasi na kupata ufaulu mzuri alieleza; (a) *Lengo la Hijja ni kumuandaa mja kumpenda Mola wake na kufuata maamrisho yake*. Katika kipengele (b) aliandika: *Chumo la*

*haramu ni kitu ambacho mtu anakuwa amechuma kwa dhulma. Hili mtu hawezi kufikia lengo la Hijja kwa sababu kwanza umemzulumu mtu na pia Yule ambae umemzulumu atakuwa hakuombei dua nzuri yani atakuwa analalamika na kuwa na kinyongo nyoyoni na wewe.* Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


9 (a) → LENGO LA HIJJAH
Ni kumfanya mja kupigania dini ya Allah (s.w) bila ya kujali chochote hata nafsi yake mwenyewe.
(b) → Jambo hayo lolote ni lengo kumchukiza na kumkasirisha Allah (s.w) Kujiunga chumo kwa njia ya haramu aidha, kuiba, kupora, kudhulumu au kupata kwa kuwa biashara haramu, mambo haya yote yana mkasirisha Allah (s.w) huwezi kufikia lengo la ibada maalum yeyote uwapo bado unamkasirisha na kumchukiza Allah (s.w) hasa unapoacha watu wanaolalamika kwa chumo lako la haramu.

Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya Majibu Sahihi ya katika Swali la 9

Katika kielelezo Na. 9.2 kipengele 9(b) mtahiniwa alijaribu kubainisha asili ya chumo la haramu na kuhusisha na malengo ya ibada maalumu, ambazo miongoni mwa ibada hizo ni Hijja.


## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne ya insha kutoka katika mada za *Dola ya Kiislamu Madinah, Sunnah na Hadithi, Qur'an na Nguzo za Uislamu.* Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu kati ya hayo. Kila swali lilikuwa na alama 15 hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 45.

### 2.3.1 Swali la 10: Dola ya Kiislamu Madinah

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza kazi nne za msikiti wa Mtume (S.A.W) kisha kubainisha jambo moja wanalojifunza Waislamu wa zama hizi kutokana na kazi hizo. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini athari za mafundisho ya Historia ya Uislamu katika maisha ya kila siku.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 61,848 (81.2%) kati ya 76,169 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 24,153 (39.1%) walifaulu kwa wastani ambapo walipata alama 5.0 hadi 9.5. Watahiniwa 20,289 (32.8%) walipata ufaulu mzuri kwakuwa walipata alama 10.0 hadi 15 na watahiniwa 17,406 (28.1%) walikuwa na ufaulu hafifu kwakuwa walipata alama 0 hadi 4.5. Chati Na. 10 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10.*

Chati Na. 10 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri, kwakuwa asilimia 71.9 waliweza kujibu kwa usahihi na kufaulu, ikilinganishwa na asilimia 28.1 watahinuiwa waliopata alama hafifu.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa umeonesha kuwa, ufaulu mzuri wa watahiniwa hao ulichangiwa na maarifa ya kutosha kuhusu Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah na uwezo wa watahini kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa hao walieleza kazi mbalimbali za msikiti wa Mtume (S.A.W) kama zilivyochambuliwa katika historia hiyo, miongoni mwa kazi hizo walizozieleza ni pamoja na;

*Kuwapokea na kuwahifadhi wageni na watu mbalimbali wa hali ya chini. (ii) Mahali pa kuswalia swala za jamaa, (iii) Taasisi ya elimu, ambapo watu mbalimbali walikusanyika na kujifunza kuhusu Uislamu kwa Mtume (S.A.W). (iv) Makao makuu ya dola ya kiislamu (ikulu), (v)*

*Kuendesha shughuli za kimahakama, (vi) Kuendesha shughuli za kibunge (Shura) (vii) Kituo cha kijeshi, (viii) Kituo kikuu cha habari kwa umma (ix) Kituo cha Afya ambapo Waislamu walikwenda kupata tiba na ushauri (x) Baitul Mal (hazina) ya dola ya Kiislamu ambapo Zakat na Sadaka zilikusanywa na kugaiwa kwa wanaostahiki.*

Baada ya kubainisha miongoni mwa kazi hizo za msikiti watahiniwa hao waliakisi mafundisho mbalimbali yaliyotokana na kuwepo kwa kazi hizo, ambapo miongoni mwake yalikuwemo;

*Tunapaswa kutafsiri upya kazi za misikiti yetu leo hii kwani misikiti mingi tuliyonayo haifanani na msikiti wa Mtume (S.A.W) si katika majengo tu bali hata dhamira za ujenzi wenyewe, (ii) Jamii ya waislamu tunapaswa kusoma kwa kuzingatia hazina ya elimu na maarifa tuliyoachiwa ili tuweze kupata nusra ya Mwenyezi Mungu (S.W) kwani changamoto tulizonazo zinatokana na ujinga na kutotekeleza ipasavyo taasisi tulizoachiwa mfano taasisi ya msikiti (iii) Waislamu tuna wajibu wa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na dini yetu kama alivyotufundisha mtume (S.A.W) katika vitendo vyake. Kitendo cha kuanza kujenga msikiti kwanza alipofika madina na kazi ambazo zilifanywa katika msikiti huo kumeacha ujumbe mkubwa kwetu ikiwa tunakusudia kufanikiwa. Na (iv) Tusitumie misikiti yetu kwa ibada maalum ya swala pekee bali ibada zingine za kijamii nazo zipewe nafasi ambazo pia ni sehemu ya kuupeleka mbele uislamu.*

Aidha, watahiniwa hao waliofaulu waliweza kufafanua vema miongoni mwa kazi zilizotajwa na kuchambua mafunzo yake stahiki kwa ufasaha. Kielelezo Na. 10.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyeweza kueleza vema miongoni mwa kazi za msikiti wa Mtume (S.A.W) na kubainisha mafunzo kwa mujibu wa kazi hizo.

10. Msikiti ni ile sehemu ya ama ni Nyumba ya ibada ya Mwenyezi Mungu (S.W) ambayo inaelezwa ni sehemu kwa ajili ya waislaam kufanyia shukhuli zao za ibada mbalimbali ikiwemo swala, kusoma Qur'an, khutba na nyenginezo. Sio sehemu ya starehe wala sehemu ya kufanyia mzaha ama mchezo wa aina yoyote ile, Allah(S.W) hulaani na hapendi kuona misikiti yake ama nyumba zake za ibada zikifanyiwa mzaha na mchezo.

Zifuatazo ni kazi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika msikiti wa bwana Mtume(S.A.W) ambazo nazo ni:-

Msikiti ulikuwa ukitumika kama ni mahakama ya waislaam; hii ni hoja ya mwanzo kabisa ambayo hutueleza kazi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika msikiti wa bwana Mtume (S.A.W) moja wapo ni hii ilikuwa ni moja ya mahakama ya waislaam pindi wakitaka kuhukumiana ama kutatuwa jambo lolote linalohusiana kuhusu dini ndipo msikiti wa Mtume(S.A.W) ndipo ambapo panapotatuliwa jambo hilo wakisimamia na swahaba au Mwenye bwana Mtume (S.A.W).

Msikiti ulikuwa ni kama sehemu ya bunge / shura kwa waislaam; na hii ilikuwa hoja ya pili ambayo hutueleza kazi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika msikiti wa bwana Mtume (S.A.W) moja wapo ni hii kulikuwa ni sehemu ya waislaam wote wanapokutana hapo na kufanyia shura / bunge lao kuhusu namna gani waweze kuondoa ukafiri kupambana na maadui wabaya ili waweze kuutangaza uislaam kwa wahusika na kwa haraka sana bila ya kuwepo pingamizi lolote lile.

Msikiti ulikuwa ni sehemu ya kujifundishi mbinu za kivita; na hii ni hojo ya tatu ambayo hutuelezea juu ya kazi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika msikiti wa bwana Mtume (S.A.W) ni ilikuwa sehemu ya waislaam ambayo walikuwa wakijifundishia mbinu za kivita dhidi ya kujikinga na maadui na makafiri ambao walikuwa wakiwaandama waislaam waweze kuwapiga na kuwa na pia kumuua kiongozi wao bwana Mtume (S.A.W) ambapo hawakuweza kufanikiwa kufanya hivyo na hatimae waislaam kuweza kuwadhibiti ipasavyo na kupata mafunzo.

Msikiti ulikuwa ni sehemu ya ibada; na hii ilikuwa hoja ya mwisho ambayo hutuelezea juu ya kazi ambazo zilizokuwa zikifanyika katika msikiti wa bwana Mtume (S.A.W) ni hii hapa ambayo ni ya muhimu ilikuwa ni sehemu ya ibada kama vile kujisomea Qur'an, kuswali na mengineyo. Ambayo hutupa faida nyingi sana na mafunzo mingi tu yatokanayo na maisha yetu kwa ujumla.

Kwa kumalizia jambo ambalo waislaam wa zama hizo walilojifunza kutokana na zama hizo ni:-

Umoja na ushirikiano wa waislaam wote kwa ujumla; na hili ndilo jambo ambalo waislaam waliloweza kujifunza waislamu wa zama hizi kutokana na kazi hizi ni waislamu wote kuwa kitu kimoja katika kufanya majambo yao bila yakuwa na woga wowote na kumtanguliza Allah (S.W) mbele juu ya kufanya maamuzi yao.

Kwa ujumla msikiti wa bwana Mtume (S.A.W) ulikuwa ukifanyika mambo mingi sana yakiwemo haya na kuleta faida nyingi sana na kutupa muongozo sisi waislaam namna gani tuweze kuishi na kutoa hofu ya kuogopa chochote tukijua kuwa Allah (S.W) yupo mbele yetu anatuongoa na kutusimamia.

Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 10

Uchambuzi zaidi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa, watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi na kupata ufaulu hafifu, walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah. Wengine walishindwa kubaini matakwa ya swali husika hivyo, walijibu kwa kubainisha mambo mbalimbali ambayo hayahusiani na msingi wa swali lenyewe.

Baadhi ya watahiniwa hao walitaja sifa mbalimbali za msikiti wa Mtume (S.A.W) kwa maoni yao badala ya kubainisha kazi nne za msikiti huo. Majibu ya watahiniwa hao yalikuwa; *Msikiti wa mtume ni mkubwa, Msikiti wa mtume ulijulikana na waislamu wote, Msikiti wa Mtume ambao Waislamu wanajivunia kuwa nao na Msikiti wa mtume ni wa kipekee katika hii dunia.* Majibu haya yaliashiria kuwa watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Watahiniwa wengine waliotoa hoja zisizo sahihi kuhusu kazi za msikiti wa Mtume (S.A.W), watahiniwa hao waliandika; (i) *Kazi ya msikiti wa mtume ni kuomba toba kwa Allah(s.w) na kusamehewa dhambi,* (ii) *Kupata swawabu na kufutiwa dhambi,* (iii) *Kufanya Sunnah katika msikiti wake,* (iv) *Kuleta ushirikiano baina ya watu.*


Vivyo hivyo, walijibu wengine kuwa; (i) *Kuleta ushirikiano baina ya watu (ii) Kuleta migawanyiko ya kazi (iii) Sehemu maalum ya kumuombea Allah (S.W), (iv) Kumuabudu Mtume wao na kumsikiliza kwa kila jambo (v) Ni sehemu ya kujinadi sana kwa ajili ya dini na Ibada.* Na wengine waliandika; *(i) Kumfanya Muislamu kumfanya Mungu yupo (ii) Kumfanya Muumini kusogea karibu na Allah (S.W), (iii) Kuifanya dini ya kiislamu kama dini ya Allah (S.W).* Hoja zilizotolewa na watahiniwa hao hazikuwa kazi sahihi za msikiti wa Mtume (S,.A.W). Hivyo zilionesha wazi kuwa walikosa maarifa kuhusu mada ya Uanzishwaji na Uendeshaji wa Dola ya Kiislamu Madinah.

Kadhalika, watahiniwa wengine waliokuwa na ufaulu hafifu, walitaja dondoo sahihi zinazojibu swali lakini hawakutoa maelezo, kwa sababu hiyo walishindwa kupata alama kamili. Miongoni mwa dondoo hizo waliandika; (i) *Kuswaliwa (ii) Kuwafundisha watu maadili mema (iii) Kuwaweka waislamu katika mtazamo mzuri wa Uislamu na (iv) Kuwa mfano wa misikiti mingi na katika Uislamu.* Baadhi katika dondoo hizi ziliwafikiana na swali lililoulizwa lakini hazikukamilishwa kwa maelezo

kama ambavyo swali la muundo wa insha linahitaji. Hivyo ilisababisha kupata ufaulu hafifu.

Vile vile, katika upande wa mafunzo yanayopatikana kutokana na kazi za msikiti wa Mtume (S.A.W), watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walishindwa kubaini mafunzo hayo kwakuwa wengi wao hawakuweza kutambua kazi halisi za msikiti huo. Baadhi yao walitaja zama na nyakati mbalimbali za uhai wa Mtume (S.A.W) kama vile; *Wakati wa mtume (S.A.W), Wakati wa uhai wa Mtume (S.A.W), Wakati wa utume wake na Wakati Mtume (S.A.W) alipokuwa anapokea utume.* Majibu hayo yaliashiria kukosa maarifa kuhusu mada iliyoulizwa hivyo wathiniwa hao walipata ufaulu hafifu.

Kwa ujumla watahiniwa waliokuwa na ufaulu hafifu katika swali hili walishindwa kujenga hoja sahihi kuhusu kazi za msikiti wa Mtume (S.A.W) na kutoa mafunzo kutokana na kazi hizo. Hivyo baadhi yao walipata alama hafifu na wengine walipata sifuri (0). Kielelezo namba 10.2 kimeonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hilo na kuchabua mafunzo yake.



10 Msikiti; ni nyumba inayojengwa kwa ajiri ya waislamu katika kumuabudu mwenyezi mungu na kufuata sunnah za mwenyezi mungu ikiwemo kusoma Qur-an. Msikiti wa Mtume (S.a.w) naeleza kazi zake zifuatazo;

Kuamasisha juu ya kumuabudu Allah; waumini walivyokuwa wakienda msikitini kwa ajiri ya ibada na ibada ikiisha huwa wanaimasisha juu ya kumuabudu mwenyezi kuwa yeye ndiye aliye umba kila kitu na pia mambo mengi kuhusu mwenyezi mungu.

Kueleza umuhimu wa swala na faida zake waislamu wengi walikuwa wanaswali bila hata ya kujua faida za swala hizo ili baada ya mtume (S.a.w) alipojenga msikiti wa wao walivyo kuwa wanaenda kuswali mtume aliambia faida ikiwepo ni ukiswali unatoka na sijida na huwa kama tochi kaburini katika nyumba ya milele.

Kuungànisha umoj; waislamu wana kutana wengi na kutoka maeneo mbalimbali katika msikiti na wakikutana wanaungana kushi-kamana katika kutimiza lengo la kumuabudu mwenyezi mungu.

Kukataza maovu na kuimarisha mema; wakikuta msikiti siku ya ijumaa katika mawaidha au siku nyengine baada ya swala huwa wanausiwa na mtume (S.a.w) au maswahaba (ra) katika kuacha maovu na kufanya mema bila ya kutarajia malipo yoyote. Kutoka kwa mtu ukamfanyi jema na kuomba msaha na kujutia kwa kufanya maovu.

Kwa ujumla; Msikiti wa mtume uliwa saidi watu wengi kujua mambo mbalimbali kuusu kumuabudu mwenyezi mungu na nyengine.


Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 10

Katika kielelezo Na. 10.2 majibu yote ya mtahiniwa yalieleza kazi mbili kubwa ambazo ni; kuelimisha na kusimamia shughuli za kijamii. Zaidi ya hapo mtahiniwa alishindwa kutaja mafundisho yoyote kutokana na kazi za msikiti huo.

### 2.3.2 Swali la 11: Sunnah na Hadithi

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha madhara manne ya kuenea kwa Hadithi maudhuu katika jamii. Swali lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kuchambua aina mbalimbali za Hadithi na athari zake katika maisha ya kila siku.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 28,562 (37.5%) kati ya 76,169 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 16,548 (57.9%) walikuwa na ufaulu hafifu kwani walipata alama 0 hadi 4.5. Watahiniwa 9,187 (32.2%) walikuwa na ufaulu wa wastani kwakuwa walipata alama 5.0 hadi 9.5 na watahiniwa 2,827 (9.9%) walikuwa na ufaulu mzuri kwakuwa walipata alama 10 hadi 15. Chati Na. 11 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 11:** *Asilimia ya Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani, kwakuwa asilimia 42.1 walifaulu vizuri ikilinganishwa na asilimia 57.9 waliopata alama hafifu.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa waliopata ufaulu mzuri umebaini kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uchambuzi wa Hadithi za Mtume (S.A.W) na mafunzo yake. Vile vile waliweza kubaini matakwa ya swali.

Watahiniwa hao waliweza kubainisha madhara mbalimbali ya kuenea kwa Hadithi maudhuu katika jamii kwa kuzingatia asili ya Hadithi hizo na mwongozo wa Qur'an na Sunnah. Miongoni mwa madhara waliyoyataja ni pamoja na;

*Kuharibika kwa mafundisho sahihi ya dini, hasa hadithi hizo zinaposambazwa na kutumiwa katika jamii* (ii) *Kuibuka kwa makundi yenye misimamo mikali (iliyo furutu ada) na kueneza uvunjifu wa amani,(iii) Kupotea kwa nguvu kazi ya vijana katika dini na jamii kwa ujumla (iv) Kuenea kwa matatizo mbalimbali ya kijamii kama maradhi, njaa na mengineyo kutokana na ghadhabu za Allah, (v) Kukua kwa mambo ya uzushi katika dini, mambo ambayo hayakuwepo wala kufundishwa na Mtume (S.A.W) na Maswahaba wake, (vi) Kuharibika kwa taswira njema ya dini ya Uislamu kama ilivyokuwa baadhi ya dini zingine.* Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.



Hadithi maudhuu. Ni hadithi zinazo mzu
lia mtume uongo, kwani hueleza kinyume na
ukweli kuhusu mtume. Hadithi hizi zilikuwa na
Mapungufu makubwa kuamia matini na wapokeaji pi
a zina Madhara Makubwa Sana katika jamii
. Yafuatayo ni madhara ya kuenea kwa hadithi hizo
Kuwafanya waislamu kutokuwa na im
ani thabiti juu ya mtume. Waislamu huweza ku
amini kwamba mtume hakuwa muadilifu
kwa kutokana na wao kuamini hadithi mau
dhuu ambazo ni hadithi zisizo na ukweli ndani yake
Huchochoa ugomvi katika jamii. Hadithi m
audhuu hupelekea ugomvi kutokana na mabish
ano juu ya hoja ya hadithi maudhu ambapo
waumini wa kiislamu huamini kwa Mtume
alikuwa ni mwenye kila tabia njema na zi
napotokea hadithi hizo kupingwa na kutoduwanga
baina ya walio zisambaza na waumini
Hupelekea kutokea kwa matabaka katika
jamii. Matabaka ambayo yataamini hadi
thi hizo na yalee yatakayo pingana na
hadithi hizo katika jamii moja ambapo kila
kundi kitaona kuwa lipo sahihi kwa jinsi linavyo
amini
Kukosa uimara katika dola za kiislamu.
Dola la kiislamu litakosa uimara kutokanana
kutongana baina ya waislamu makundi kwa
makundi yenye itikadi tofauti tofauti. Ampapo
huenda pasinge kuwepo hadithi maudhuu. Uislamu
katika jamii ungekuwa na nguvu kwani itikadi
ingekuwa ni moja tu.
Kwahiyo, hayo ni baadhi tu ya madhara
ya kuenea kwa hadithi maudhuu katika jamii
na pengine hadithi hizo zingeweza kupingwa
na kutokukubalika kabaina ya waumini pasinge
tokea matabaka baina ya waislamu ulimwe
nguni kote. Pia hatupaswi kuamini hadithi
mau

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 11.

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu walishindwa kujibu swali hili kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha na kushindwa kubaini matakwa ya swali.


Baadhi ya watahiniwa hao waliandika; *Kumuuliza Mtume maswali ya uzushi, Walimzushia Mtume (S.A.W) maneno machafu yenye kuchukiza, Kuhifadhi hadithi za uongo, Kukosekana kwa wapokezi na wasimulizi wa Hadithi.* Mwingine aliandika; *Hadithi maudhuu inapingana na Qur'an, Kusema uongo, Kumsengenya mtu, Kudumaza jamii.* Majibu hayo yaliashiria kueleza sifa za Hadithi badala ya kueleza madhara ya

kuenea kwa Hadithi maudhuu. Hivyo watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali.

Kadhalika, watahiniwa wengine walioshindwa kujibu swali hili ipasavyo waliandika; *Kuweka kituo kati ya aya moja na nyingine wakati unasoma Kuruani, Kuanza na authubillahi mina shaitwani rajimu unapoanza kusoma Qur'an, kusoma aya moja hadi nyingine wakati unasoma Qur'an*. Majibu hayo yaliashiria kueleza adabu za kusoma Qur'an badala ya kueleza madhara ya Hadithi maudhuu.

Kundi lingine la watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi walitoa hoja ambazo hazikuhusiana na athari za Hadithi maudhuu kwa ujumla, miongoni mwao aliandika; *Kutojua kusoma Hadithi, Kutojua lengo la Hadithi, Kutojua faida au umuhimu wa Hadithi*. Majibu hayo yaliashiria kuwa mtahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Hadithi maudhuu kwa ujumla.

Baada ya kuangazia majibu mbalimbali yaliyotolewa na watahiniwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, uchambuzi ulibaini kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Sunnah na Hadithi hususani aina mbalimbali za Hadithi na sifa zake. Hayo yalidhihirika katika hoja walizotumia watahiniwa katika kujibu swali ambazo hazikuonesha uhusiano na dhana ya Hadithi maudhuu. Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


11 Bainisha madharo manne ya kuenea kwa hadithi maudhui katiko jamii

Kutoa maneno yasiyo yakweli : watu wengi wanaamini kuwa hadithi hizi zio ko kweli ndo mana zinaenea kwa kasi na watu kusema maneno yasiyo ya kweli

Maneno ambayo au hadithi ambayo haifuati taratibu zote zina leto madharo kushughulikia kwano mtume hakufundisha mafunzo ya hadithi ii hadithi hizi zinaenda kinyume na maneno ya mtume

Sina too taarifa zisizo za kweli. nisio za kweli kwasababu hazina khaldi wa vitabu walo maneno menyewe ni yauongo ni maneno au ni hadithi ambayo hazielewezi amboro hazina tako mwanzo

Zina utofauti wa matendo ya mtume na sunna azozifundisha mtume mohamadi SWALLAH ALLAH ALLAW WASALAMU. ni sio zo kwelr zinaficha mambo mengi zinakuwa hazina ukweli wa ndani zinakuwa hazieleweki zinaendo kinyume na mafundisho YA Quruan na sunna?


Kielelezo Na. 11.2 Sampuli ya Majibu yasiyo Sahihi katika Swali la 11

Katika kielelezo Na. 11.2 mtahiniwa ameeleza hoja zinazoashiria sifa za Hadithi maudhuu badala ya madhara ya Hadithi hizo. Mtahiniwa huyo alishindwa kubaini matakwa ya swali.

### 2.3.3 Swali la 12: Qur’an

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza mambo matano ya kuzingatia katika usomaji wa Qur’an ili iwe mwongozo wa maisha ya Muislamu. Swali hili lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutumia ujuzi walioupata katika kuisoma Qur’an vilivyo.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 67,525 (88.7%) kati ya 76,169 (100%) walifanya swali hili. Kati yao, watahiniwa 51,168 (75.8%) walikuwa na ufaulu hafifu kwakuwa walipata alama 0 hadi 4.5. Watahiniwa 14,900 (22.1%) walikuwa na ufaulu wa wastani ambapo walipata alama 5.0 hadi 9.5 na watahiniwa 1,457 (2.2%) walikuwa na ufaulu mzuri kwakuwa walipata alama 10.0 hadi 15. Chati Na. 12 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.




**Chati Na. 12**: *Alama za watahiniwa kwa asilimia katika swali la 12*

Chati Na. 12 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa ulikuwa hafifu, kwakuwa asilimia 75.8 ya watahiniwa hao walishindwa kujibu kwa usahihi na kupata ufaulu wa chini, ikilinganishwa na asilimia 24.2 ya watahiniwa waliofaulu vizuri.

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa waliopata alama hafifu umeonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa hao walishindwa kubaini matakwa ya swali husika na wengine hawakuwa na maaarifa ya kutosha kuhusu mada ya usomaji wa Qur'an. Majibu ya watahiniwa hao yalitofautina baina ya kuchanganya adabu za usomaji wa Qur'an na hoja za makafiri dhidi ya Qur'an ambayo ni kinyume na mambo muhimu ya kuzingatia katika usomaji Qur'an ili iwe muongozo wa maisha.

Watahiniwa waliandika hoja kama vile; *Kuanza kwa kumlaani sheitwani*, *Kufuata hukmu mbalimbali*, *Kusoma Qur'an kwa sauti nzuri. Kuanza na Bismillahir Rahmaanir Rahiim*, *Kuwa na stara*, *Kuwa*

*tohara, Kuwa mnyenyekevu kwa Allah.* Na wengine waliandika; *Ukisoma Qur'an uwe hauna hedhi, Ukisoma Qur'an uwe hauna janaba, Ukisoma Qur'an uwe hauna uchafu wowote, Ukisoma Qur'an uwe umevaa kitambaa kichwani.* Majibu hayo yalionesha kuwa watahiniwa walishindwa kubaini matakwa ya swali husika. Hivyo badala ya kueleza njia za usomaji wa Qur'an kama muongozo wakaeleza adabu za usomaji wa Qur'an.


Vivyo hivyo, watahiniwa wengine walieleza matokeo ya herufi katika usomaji wa Qur,an, kama vile; *Ulimini, Matendoni, Puani, mdomoni na kooni.* Majibu hayo yaliashiria kueleza hukumu za Tajwiid badala ya njia za usomaji wa Qur'an kama mwongozo.

Kadhalika, wengine walitoa kama vile; *Qur'an ni mashairi yaliyotungwa na Muhammad (s.a.w) ili kuwatungia waislam. Quran ni zao la njozi za Mtume (s.a.w) zilizovurugika katika ndoto, Qur'an ni zao la anaetaka ufunuo kutoka kwa Allah (s.w).* Majibu hayo yaliashiria kueleza hoja za Makafiri dhidi ya Qur'an tofauti na matakwa ya swali husika.

Katika mrengo huo huo, wengine walieleza faida za usomaji wa Qur'an katika jamii, kama vile; *Qur'an inasaidia waumini kuleta toba ya kweli, Inasaidia wanajamii kujiepusha na maovu, Husaidia kutatua baadhi ya matatizo katika jamii, Inawaongezea waumini imani, Kuelimisha jamii*. Na wengine walieleza uthibitisho wa Qur'an kuwa ni maneno ya Allah (S.W) kwa mujibu wa Qur'an yenyewe, nao walieleza kuwa; *Qur'an inajieleza yenyewe, Kukosolewa kwa mtume ndani ya Qur'an, Kushuka kwa miaka 23, Kushuka kwa mpangilio na Qur'an kushuka kidogokidogo.* Hoja zote hazikujibu swali kwakuwa hazielezi dhana ya usomaji wa Qur'an kama mwongozo wa maisha ya Muislamu.

Baadhi ya watahiniwa walionesha kutokuwa na maarifa kuhusu mada za Qur'an, hivyo walieleza dondoo mbalimbali ambazo hazikuwa na uhusiano na swali husika na nyingine zilikuwa dhidi ya Qur'an yenyewe. Miongoni mwao aliandika; *Kuiamini Qur'an wakati wa usomaji, Ujuzi wa usomaji wa Qur'an, Lengo la usomaji wa Qur'an, Kuwe na imani na nia katika usomaji wa Qur'an.* Mwingine aliandika; *Mwanzo wa Qur'an, Matumizi ya Qur'an, Kuzingatia jinsi irabu zilivyowekwa.* Majibu hayo ya watahiniwa kwa ujumla yaliashiria kutofahamika vema kwa mada ya usomaji wa Qur'an. Hivyo,

walishindwa kubaini hoja sahihi za swali. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.


12 Qur-an :- Ni chemchem ya maisha ya mwanadamu
Ni kweli kwamba murambambi ya kuzingatia katika usomaji wa qur-an ili iwe muongozo wa maisha ya muislamu kwasababu Qurani-ni kitabu cha mwenyezimungu na kimeletwa ili kuwa muongozo wa maisha ya mwanadamu. yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika usomaji wa qur-ani.
Qur-ani imejielezea yenyewe :- kwasababu tunaona kwa qur-ani ni kitabu cha Allah (sw) inachotoa muongozo juu ya maisha ya binaadam ya kibinafsi na kijumii.
kukosolewa kwa mtume ndani ya qur-an :- kwasababu watu watukuwa wanadai kwamba qurani ameiandika muhammad wakati ni ya Allah na Allah amemkosoa alipo kosea hivyo sio kitabu cha muhammad.
kushuka kwa miaka 23 :- Imeshuka kwa miaka 23 kwasababu inashuka kutokana na matukio ndo maana imechukuwa miaka mingi
kushuka kwa mpangilio :- quran imeshuka ivyo ili watu waweze kupata ujumbe kamili kwa haraka na kukikana na matukio fulani.
Qur-ani kushuka kidogo kidogo :- kwasababu ili waweze kupanga kama ilivyo bilo ya kuchanganya na kuhikana na matukio mbalimbali
Hitimisho :- Tunatakiwa kufuata kitabu cha Allah ambacho ni quran ili kupata muongozo kamili wa maisha yetu hapa duniani na kesho akhera.

Kielelezo Na. 12.1 Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 12

Katika kielelezo Na. 12.1 mtahiniwa ameeleza hoja zinazothibitisha Qur'an kuwa ni kitabu cha Mwenyezi Mungu (S.W) badala ya kueleza yanayopaswa kuzingatiwa katika usomaji wa Qur'an ili iwe mwongozo wa maisha ya Muislamu. Mtahiniwa alishindwa kubaini matakwa ya swali

Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa wachache waliofaulu katika swali hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana mbalimbali za usomaji wa Qur'an na kuelewa vema matakwa ya swali hilo. Watahiniwa hao walieleza dondoo za kuzingatia katika usomaji wa Qur'an kama mwongozo wa maisha ya Muislamu kwa ufasaha na ufafanuzi uliotosheleza. Wengine kati yao, walichanganya baadhi ya hoja zilizokuwa sahihi na zisizo sahihi.

Miongoni mwa hoja walizotoa watahaniwa hao zilikuwa; (i) *Kuzingatia lengo la Qur'an*, (ii) *Kuzingatia mafunzo yatokanayo kwenye Qur'an, ,* (iii) *kuzingatia tafsiri ya Qur'an (iv) Kuzingatia mafunzo yatokanayo kwenye Qur'an (v) Kuitumia Qur'an katika maisha yetu yote (vi)Kuijua lugha yake ili kupata maana halisi ya yale unayoyasoma na kuondokana na kuisoma Qur'an kikasuku. (vii) kuiwekea mikakati ya kiutekelezaji kila tunaposoma aya chache zenye maelekezo ya kiutendaji kama vile kusimamisha swala, kusimamisha uadilifu, Zakat n.k. (viii) Kujifanyia tathmini kila baada ya muda ili kubaini kama Qur'an imekubadilisha kitabia na kuathiri watu waliokuzunguka.* Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali hili.

12. Qur-an ni chemichemi za sheria katika uislamu. Ni muongozo wa maisha ya mwanadamu kwani kumfundisha kutumia mbinu nyingi katika historia zilizopita kuhusu kujikisha katika eneo na sehemu hizi. uislamu. Pia ni kitabu kisichokuwa na mfano pamoja na mabadiliko kutokana na zama mpya. Zifuatazo ni mambo ya kuzingatia katika usomaji wa Qur-an. kuwa muongozo wa maisha.

Kuzingatia lengo la Qur-an. Hili ni jambo kubwa sana maana kila kukisoma kitu bila ya kujua lengo la Qur-an ni nini. Hasa pale ambapo unaaza kusoma kitabu husika. Watu wengi hupenda kujua lengo la kitu kisha kufuata. Mfano lengo la Qur-an ni muongozo kwahiyo lazima kulizingatia.

Kuzingatia sheria zinazofundishwa kwenye Qur-an. Hii pia ni jambo la kuzingatia hasa sheria zilizotolewa nayo kama muongozo wa maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni. Kila mtu huwa lazima afuate sheria ili kufuata kile achopaswa kujua maana kila kitu kukiendea au kuwa muongozo ni sheria.

Kuzingatia mafunzo yatokanayo kwenye Qur-an. Hata kufuata muongozo yapaswa kupata funzo litokanalo na jambo husika. Mfano Qur-an humuwezesha muislamu kujikisha lengo lako. Kwani mafunzo yote ya Qur-an ni mafunzo yanayomuongoza mwanadamu katika kila kipengele cha Maisha yake.

Kuzingatia maamrisho na makatazo yatokanayo na Qur-an. hii nayo ni miongoni mwa mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa katika maisha yako hapa duniani. Kwani muislamu anaweza kufanya mambo mengi mazuri katika hasa aliyoamrisha Allah<s.w> na kujiepusha na makatazo yatokanayo na Qur-an kwani sio mambo mazuri. Kwani ni muongozo wa maisha.

Kuzingatia tafsiri ya Qur-an. hii ni miongoni mwa mambo yanayopaswa kuzingatiwa. Kwani tafsiri ya Qur-an ndo nyenzo pekee ya msomaji kuelewa zaidi kama sehemu ambayo anaweza kuona muongozo wa Qur-an. Pia ni matini ya lugha ya kiarabu baada ya kujua tafsiri huwa ni nyepesi kuifuata.


Kwahiyo hizo ndizo mambo ambayo kuzingatia msomaji wa Qur-an kwa muongozo wa maisha. Sasa yapaswa kutufundisha au kujifunza Qur-an vizuri zaidi na kuitunza vizuri na kuifuata kwani ni muongozo.

Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 12

### 2.3.4 Swali la 13: Nguzo za Uislamu

Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kufafanua faida nne zinazopatikana katika jamii itakayosimamisha Swala za jamaa. Swali hili lilikusudiwa kuwapima watahiniwa umahiri wa kutathmini athari za Swala za jamaa katika jamii.

Watahiniwa 70,305 (92.3%) kati ya 76,169 (100%) walifanya swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 37,981 (54.0%) walikuwa na ufaulu hafifu kwakuwa walipata alama 0 hadi 4.5. Watahiniwa 23,642 (33.6%) walipata ufaulu wa wastani ambapo walipata alama 5.0 hadi 9.5 na watahiniwa 8,682 (12.3%) walikuwa na ufaulu mzuri kwakuwa walipata alama 10 hadi 15. Chati Na. 13 inaonesha muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa hao kwa asilimia.





**Chati Na. 13:** *Asilimia za Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Chati Na. 13 inaonesha kuwa ufaulu wa watahiniwa katika swali ulikuwa wa wastani, kwakuwa asilimia 46.0 walifaulu vizuri ikilinganishwa na asilimia 54.0 ya waliopata alama hafifu.

Uchambuzi uliofanyika kwa watahiniwa waliopata ufaulu mzuri ulibaini kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Kusimamisha Swala za jamaa. Aidha, waliweza kufafanua faida mbalimbali za kijamii za Swala hizo kwa kuzingatia malengo ya Swala

kwa ujumla na mafundisho mbalimbali yaliyomo katika Qur'an na Hadithi za Mtume (S.A.W).

Miongoni mwa faida walizoeleza watahaniwa hao zilikuwa; *(i) Kuitakasa jamii kimwili na kiroho, (ii) Kuimarisha udugu na mapenzi baina ya Waumini (iii) kuondoa bughuza baina ya Waumini (iv) Kujifunza uongozi bora na mahusiano mema baina ya kiongozi na wanaoongozwa, (v) kuimarisha utaratibu wa kusoma na kusikiliza Qur'an, (vi) Fursa ya kukumbushana mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika maisha yetu, (vii) Kupata utulivu na furaha (burudani) kwa kukutana na waumini wenzako, (viii) Jukwaa la kutatua changamoto mbalimbali za Waumini, (ix) Ni fursa ya kuwafundisha vijana swala kwa vitendo.* Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuzingatia matakwa ya swali.


13 Swala za jamaa ni swala amb-
azo zina swaliwa kwa pamoja msikitini zikiong
ozwa na imam, Imam ndiye anaye ongoza swala
hizo za jama Swala ya jamaa ina anza na
watu kwanzia wawili na kuendelea kuwe na
Imam na maamum. zifuatazo ni faida za
kuswali swala za jamaa.
Kuwafunza waislam Uongozi bora
Swala za jamaa huwafunza waumini jinsi
ya kuwa kiongozi bora na njia bora ya kong
oza watu katika jamii
Kuimarisha mshikamano baina ya
wanajamii - Swala za jamaa zina imari
sha mshikamano baina ya wanajamii
kuzidi kuwa na mshikamano mzuri bain
baina yao.
Kuimarisha amani na Upendo
kwa wanajamii miongoni mwa faida
za kuswali swala ya jamaa ni kuimarisha
amani na Upendo kati ya wanajamii
Kuwafunza waislam nidham na
Utii kwa viongozi wao. pia swala za jam
aa zina wafunza wailam pamoja na
waumini kuwa na nidham na utii kwa
viongozi wao.
Kuwafanya watu kuwa wamoja
na kumshinda sheitwani Swala za jamaa
huwafanya waumini kuwa na mshikama
no na kumshinda ibilis sheitwani.
Kwa kumalizia ni bora zaidi kwa
waumini kuswali swala za jama kutokana
na faida za jamaa kuliko kuswali mmoja mmoja.

**Kielelezo Na**. 13.2: Sampuli ya Majibu Sahihi katika Swali la 13


Uchamuzi zaidi ulibaini kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu walishindwa kujibu swali hili kwa sababu ya kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Kusimamisha Swala za jamaa na wengine kushindwa kubaini matakwa ya swali husika. Hivyo walishindwa kujibu kwa usahihi katika swali hili.

Sababu za watahiniwa wengi kupata alama za chini katika swali hili ni kutoelewa matakwa ya swali, kujitungia maswali pamoja na kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya swala za jamaa. Aidha, uchambuzi zaidi umefafanua sababu za watahiniwa hao kupata alama za chini kama ifuatavyo:

Baadhi ya watahiniwa hao waliandika yafuatayo kuwa; *Swala za jamaa huswaliwa kwa wakati na muda maalum, Swala za jamaa huswaliwa kwa Sunnah, Swala za jamaa huongeza idadi ya vipindi, Swala za jamaa kwa siku moja tu kila wiki*. Wengine walijibu; *Watapata kuwekwa shura (vikao), Watapata kukimbilia mambo ya kheri, Watapata kufanya kazi zao kwa pamoja, Watapata kwenda madrasa (chuoni).* Na wengine; *Kuepukana na dhambi ndogondogo na kubwa wakati wa swala ya jamaa, kumjua Mwenyezi Mungu kila unapokuwa, Kuwa karibu na Mwenyezi Mungu, Kunusurika misukosuko ya kimaisha.* Majibu hayo yaliashiria kuwa watahiniwa hao hawakuifahamu hata dhana ya “Swala ya jamaa” yenyewe ambayo walitakiwa kuonesha umuhimu wake.

Wengine walijibu: *Kunufaika na maisha ya akhera, kupunguzwa adhabu za kaburini, kupata maghfira kutoka kwa Allah (s.w), Husaidia kuwa na upeo wa kumuamini Allah (s.w) kwa kila jambo.* Mtahiniwa mwingine akaandika; *Watajiepusha na machafu na maovu, watakuwa wanaswali kwa wakati, watapata Swala za Sunnah na watu watapata khushui.* Wengine walijibu kuwa; *Kuepukana na matendo maovu, Kuwaombea waislamu, Kuepuka unafiki na umbeya, Kuwaongoza waislamu, Kuwa na tabia njema.* Mwingine alijibu*:-Kuwapa khofu ya kuwa karibu na Allah (s.w), Kupata neema bila shida, kumuandaa kwenda peponi, Kuwajengea khofu ya kulipwa kwa Allah (s.w).* Watahiniwa hawa walieleza baadhi ya faida binafsi za Swala hiyo badala ya faida za jamii.

Watahiniwa wengine walijibu*:-Kuwaombea wale wote waliotangulia, Kujumuika wote katika swala ya jamaa, Kumpwekesha Allah (s.w), Kuwa na maadili yaliyo mema, Kuwajenga waja kuwa na imani na kumtumikia Allah (s.w).* Majibu hayo yaliashiria kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya Swala za Jamaa. Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali kwa usahihi.


13. Faida: ni kila kitu mtu anachokipata katika jambo analokuwa amelikusudia au amelifanya ili kumnufaisha katika mambo yake. Zifuatazo ni faida zitakazopatikana katika jamii itakayosimamisha swala za jamaa.

Kupata thawabu kwa Allah; watu watakao simamisha swala za jamaa watapata thawabu kwa allah (s.a.w) kwa sababu Allah ndio muweza wa kila kitu katika hii dunia.

Kupata baraka kwa Allah; watu watakao simamisha swala ya Jamaa watapata baraka kutoka kwa Allah na pia atawabariki kwa kila kitu.

Kupata kujengewa pepo kwa mwenyezimungu; Jamii itakayo simamisha swala ya Jamaa kama mtume (s.a.w) alivyo sema wa tajijengea pao katika mbigu yake Allah.

Kupata baraka kwa kila kitu watakacho muomba mwenyezimungu; Allah amesema watakao simamisha swala ya Jamaa na wakaniomba kitu hakika watapatikiwa. Hivyo basi swala ya Jamaa katika jamii yetu hii ni ya muhimu ili kuweza kupata mambo muhimu kutoka kwa Allah.

Hitimisho; Zipo faida nyingi zinazopatikana katika jamii itakayo simamisha swala ya Jamaa na baadhi ya faida nimeweza kuzitaja ni kama kupata baraka kwa mwenyezimungu, kupata thawabu na zipo nyingi faida zinazopatikana katika jamii itakayo simamisha swah ya Jamaa.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 13

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu mwaka 2021 ulikuwa na maswali kumi na tatu (13) yaliyotolewa katika mada kumi na nane (18). Swali la kwanza liliundwa na mada kumi na mbili (12) ambazo ni; *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu*, *Imani ya Kiislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu*, *Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Fiqh, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Qur'an, Sunna na Hadithi, Nguzo za Uislamu, Historia katika Uislamu,* na *Bara Arab zama za Jahiliyyah*, ambapo ufaulu wa jumla katika mada hizo ulikuwa mzuri (79.6%).

Tofauti na swali la kwanza ambalo liliundwa na mada mbalimbali, maswali mengine kumi na mbili (12) kila moja lilitoka katika mada mahususi. Aidha, ufaulu katika mada hizo hulikuwa mzuri katika mada moja tu *Dola ya Kiislamu Madinah* ambayo ilikuwa na ufaulu wa asilimia 71.9.

Zaidi ya hapo, mada nne (4) zilikuwa na ufaulu wa wastani, ambazo ni; *Nguzo za Uislamu (49.6%), Sunnah na Hadithi (42.1%) Familia ya Kiislamu (38.6%)* na *Mfumo wa Jamii ya Kiislamu (33.8%).* Kadhalika, mada nne zingine (4) miongoni mwa zilizopimwa zilikuwa na ufaulu hafifu, ambazo ni; *Qur'an (16.3%), Haki na Uadilifu Katika Uislamu (14.1%) Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W) (6.9%)* na *Nguzo za Imani (6.0%).*

Ufaulu mzuri katika mada ya *Dola ya Kiislamu Madinah* ulichangiwa na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha na kubaini matakwa ya swali lililoulizwa. Ama, ufaulu wa wastani katika mada nne (4) zilizo orodheshwa, ulichangiwa na uelewa mdogo wa watahiniwa uliosababisha kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yao na wengine kushindwa kufafanua vema hoja sahihi walizotoa katika majibu yao.

Aidha, mada nne (4) zilizokuwa na ufaulu hafifu, zilisababishwa na watahiniwa kushindwa kujibu maswali waliyoulizwa kutokana na kukosa na maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine kushindwa kubaini matakwa ya maswali hivyo, walishindwa kujenga hoja sahihi katika kujibu maswali.

Muhtasari wa ufaulu katika mada umeoneshwa katika Kiambatisho cha pekee, ambapo rangi ya kijani imetumika kubainisha mada zenye ufaulu

mzuri, rangi ya njano imetumika kubainisha mada zenye ufaulu wa wastani na rangi nyekundu imetumika kubainisha mada zilizo na ufaulu hafifu.

## 4.0 HITIMISHO

Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2021 somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kilikuwa cha wastani, ambapo asilimia 47.09 ya watahiniwa walifaulu. Aidha, uchambuzi umeonesha changamoto mbalimbali ambazo zinapaswa kutatuliwa ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mitihani ijayo. Changamoto zilizoonekana katika mtihani huu ni pamoja na watahiniwa kukosa maarifa ya kutosha katika mada mbalimbali kama vile; *Qur'an (16.3%), Haki na Uadilifu Katika Uislamu (14.1%), Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W)(6.9%)* na *Nguzo za Imani (6.0%)*. Kadhalika, kushindwa kubaini matakwa ya maswali, kushindwa kujenga hoja na kuzifafanua ipasavyo (hususani katika maswali ya majibu mafupi) pia kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika kujibu maswali.

Ili kuinua zaidi kiwango cha ufaulu kwa mada zote katika mitihani ijayo, jitihada za ziada zinahitajika kufanywa katika mchakato wa ufundishaji, ujifunzaji na upimaji endelevu wa wanafunzi shuleni. Jitihada hizo zinapaswa kulenga kuwajengea wanafunzi maarifa ya kutosha juu ya mada za somo ili wawe na uwezo wa kuelewa matakwa ya maswali na kujenga hoja stahiki.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuweza kuinua kiwango cha ufaulu katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu wanapaswa kuzingatia matumizi ya vitabu vya kiada na mbinu shirikishi katika ufundishaji ili kufikia umahiri uliyokusudiwa katika kila mada.

(b) Walimu wanapaswa kuwapima wanafunzi kwa muundo wa maswali ya umahiri yanayozingatia nyanja za juu za ufahamu ili kuimarisha uwezo wa wanafunzi na kuendana na mabadiliko yaliyopo.

(c) Wanafunzi wanapaswa kuzingatia mbinu za kusoma kwa kuelewa ili kuwa na uwezo wa kujenga hoja sahihi na kuzifafanua ipasavyo.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

| Na. | Mada | Ufaulu wa Kila Swali | | Asilimia ya Watahiniwa walio na wastani wa 30 na zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | |
| 1 | Mtazamo wa Uislamu Juu ya Elimu, Imani ya Kiislamu, Kumjua Mwenyezi Mungu, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Dini, Fiqh, Mtazamo wa Uislamu Juu ya Ibada, Mambo ya Lazima Kufanyiwa Maiti Muislamu, Qur'an, Sunna na Hadithi, Nguzo za Uislamu, Historia katika Uislamu, Bara Arab zama za Jahiliyyah. | 1 | 80.2 | 80.2 | Vizuri |
| 2 | Dola ya Kiislamu Madinah | 10 | 71.9 | 71.9 | Vizuri |
| 3 | Nguzo za Uislamu | 2 | 79.0 | 49.6 | Wastani |
| | | 9 | 23.8 | | |
| | | 13 | 46.0 | | |
| 4 | Sunnah na Hadithi | 11 | 42.1 | 42.1 | Wastani |
| 5 | Familia ya Kiislamu | 5 | 38.6 | 38.6 | Wastani |
| 6 | Mfumo wa Jamii ya Kiislamu | 4 | 33.8 | 33.8 | Wastani |
| 7 | Qur'an | 12 | 24.2 | 16.3 | Hafifu |
| | | 8 | 8.3 | | |
| 8 | Haki na Uadilifu Katika Uislamu | 6 | 14.1 | 14.1 | Hafifu |
| 9 | Historia ya Uislamu Baada ya Kutawafu Mtume (S.A.W). | 7 | 6.9 | 6.9 | Hafifu |
| 10 | Nguzo za Imani | 3 | 6.0 | 6.0 | Hafifu |
| **Wastani wa Jumla wa Ufaulu katika Mada** | | | | **35.95** | **Wastani** |